epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US
Jumatatu Aprili 15, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581647
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital



UKURASA 22

**GUARDIOLA: TUNAWANIA MATAJI MA3**

**Lori** lingine la mafuta laanguka, wananchi wachota mafuta, wanaswa UK.2

**Wataka** hatua udhalilishaji wa wanawake mitandaoni UKURASA 5

MAKONDA ASHTUKA

**Aliyelipa** kodi mil. 24/- apewa risiti ya mil. 3/- UK. 20



**Dk. Mwinyi asema kero za Muungano zinatafutiwa dawa**

UKURASA 3

# Milima miwili yaporomoka

• **Ni** ya mikoa miwili, nyumba, shule, barabara zafunikwa tope; watu 36,000 wahitaji msaada Rufiji... *Endelea Uk. 2*



Moja ya nyumba za wakazi wa Kata ya Itezi, jijini Mbeya, ikiwa imezingirwa tope baada ya Mlima Kawetere, kumeguka na kusababisha maporomoko ya tope lililofunika zaidi ya nyumba 20 na shule, jana asubuhi. **PICHA: NEBART MSOKWA**



Majeneza yenye miili ya wanafunzi wanane wa Shule ya Msingi Ghati Memorial na mmoja wa waokoaji waliofariki dunia kutokana na ajali ya gari, ikiwa katika viwanja vya Shule ya Sekondari Sinoni, jijini Arusha jana, kwa ajili ya kuagwa. Ibada iliongozwa na Askofu Mkuu Jimbo Kuu Katoliki Arusha, Isaack Aman. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**



Nchimbi Kinana

# Kinana, Nchimbi wafunda wanachama CCM mikoani

UKURASA 20

**MICHEZO** **YANGA SC, AZIZ KI WANOGA KILELENI** UK.24 **KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA

# Milima miwili yaporomoka

Na Mwandishi Wetu

ZAIDI ya watu 58 wamefariki dunia katika matukio tofauti ya mafuriko yaliyosababishwa na mvua inayoendelea kunyesha maeneo mbalimbali nchini, huku milima miwili ikiporomoka na kusababisha madhara katika mikoa ya Njombe na Mbeya.

Jana, Msemaji wa Serikali, Mobhare Matinyi, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam alisema vifo hivyo ni katika mikoa ya Arusha (10), Dar es Salaam (2), Geita (4), Iringa (5), Kilimanjaro (1), Lindi (4), Mbeya (6), Morogoro (5), Pwani (11) na Rukwa (10).

Alisema maafa makubwa zaidi yako mkoani Pwani katika Wilaya ya Rufiji na Kibiti ambako kata 17 (12 za Rufiji na tano za Kibiti) zimeathiriwa zaidi.

Alisema Morogoro kuna kata 50 zilizoathirika (Malinyi kata nane, Mlimba tisa, Ulanga nane, Ifakara tisa na Halmashauri ya Mkoa Morogoro kata 22.

Matinyi alisema nyumba zilizoathirika katika mikoa hiyo miwili ya Pwani na Morogoro ni 8,532; Pwani nyumba 628 na Morogoro nyumba 7,904 pamoja na mashamba yenye ukubwa wa jumla ya ekari 76,698 (Morogoro ekari 34,970 na Pwani ekari 41,728).

Alisema zilizoathirika katika maafa hayo kwa ujumla wake ni 10,839 (kaya 4,635 mkoani Pwani na 6,204 mkoani Morogoro).

Pia kuna uharibifu wa miundombinu ya makaravati, madaraja na barabara, hivyo kuathiri huduma za usafiri na usafirishaji na upotevu na mali huku mifugo ikikosa malisho.

Matinyi alisema tayari serikali imechukua hatua mbalimbali na watu waliookolewa ni 2,278. Kati yao, Morogoro ni 78 na Pwani 2,200.

Alisema serikali imeanzisha kambi nane kwa waathirika zenye watu 1,529. Kati yake, saba zina watu 1,394 mkoani Pwani na moja yenye watu 135 mkoani Morogoro ambako wanatoa huduma muhimu zikiwamo za afya.

**MBEYA**

Wanafunzi 200 wa Shule ya Msingi Generation iliyoko Kata ya Itezi, jijini Mbeya, wamenusurika kifo baada ya mabweni walimokuwa wanalala kufukiwa na tope lililotokana na kuporomoka kwa Mlima Kawetere kutokana na mvua inayoendelea kunyesha.

Tope hilo lililoporomoka jana limefunika nyumba 20 za makazi ya wananchi na kusababisha zaidi ya wananchi 200 kukosa makazi, huku dalili zikionyesha mlima huo kuendelea kumeguka.

Tukio hilo lilitokea asubuhi wakati baadhi ya wananchi wakiwa ndani ya nyumba na wengine wakiwa kanisani huku wanafunzi wa Shule ya Generation wakiwa shuleni huko. Waliondolewa kabla mabweni yao hayajafunikwa.

Diwani wa Kata ya Itezi, Sambwee Shitambala alisema tukio hilo limesababishwa na uharibifu wa mazingira kwenye mlima huo hasa ukataji miti ovyo, shughuli za kilimo na ujenzi wa makazi maeneo ya milimani.

Kamanda wa Jeshi la Zimamoto Mkoa wa Mbeya, Mrakibu wa Zimamoto, Malumbo Ngata alisema kuwa baada ya kupata taarifa za tukio hilo walikwenda katika eneo hilo kwa ajili ya uokoaji.

Alisema walianza kuwahamisha watu ambao walikuwa wapo kwenye nyumba zao na kuwapeleka maeneo salama na kwamba hakuna kifo cha mtu yeyote kilichotokea kwenye eneo hilo. Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera aliagiza wananchi watakaokosa makazi watafutiwe maeneo salama na masomo yasitishwe katika Shule ya Generation pamoja na ya St. Mary's ambayo iko jirani.

**KILIMANJARO**

Jana zaidi ya abiria 1,500 wa safari za usiku na mchana kutoka na kuingia mikoa ya Kanda ya Kaskazini na kwenda mikoa ya Kanda ya Kati, Kanda ya Ziwa, Dar es Salaam na Morogoro, walisota barabarani kwa saa saba, wakisubiri barabara kuu ya Arusha-Moshi kufunguka, baada ya magogo makubwa, mawe na maji kuifunga kutokana na mvua, Meneja wa TANROADS, Motta Kyando alithibitisha.

**KATAVI**

Mvua ilioanza kunyesha saa tisa usiku wa kuamkia jana katika Manispaa ya Mpanda, mkoani Katavi ilisababisha watu kushindwa kuendelea na shughuli zao huku abiria waliokua wakisafiri kuelekea mkoani Kigoma na vijiji vilivyoko wilayani Tanganyika wakishindwa kuendelea na safari kutokana na daraja kujaa maji. Diwani wa Misunkumiro, Alfred Matondo alitoa taarifa kuwa zaidi ya nyumba 30 zimezingirwa na maji.

**NJOMBE**

Katibu Tawala wa Mkoa wa Njombe, Judica Omary, alisema jana kuwa mvua kubwa imesababisha uharibifu wa miundombinu kwa kukatisha mawasiliano kati ya Makete na Ludewa.

Alisema kwenye barabara ya Ikonda -Lupila -Mlangali kuna maporomoko ya udongo ya mlima katika Kijiji cha Masisiwe wilayani Makete na kuwataka wananchi kuchukua tahadhari wakati TANROADS wakufungua eneo hilo ambalo limeonyesha dalili ya maporomoko zaidi.

**KIBITI**

Mkuu wa Wilaya ya Kibiti, Kanali Joseph Kolombo jana aliomba wadau kujitokeza kusaidia waathirika wa mafuriko ambao nyumba zao zimezingirwa na maji kutokana na mvua kubwa inayoendelea kunyesha.

"Wadau mbalimbali kama taasisi na watu binafsi popote mlipo, ninaomba mwitizame Kibiti kwa jicho la tatu, waathirika hawa wana uhitaji mkubwa, hali si nzuri kwa sasa, misaada ya kibinadamu inahitajika.

"Mpaka sasa tuna jumla ya waathirika 36,900 ambao mbali na nyumba zao kufurika maji, wapo pia waliopoteza mashamba yao," alisema.

***Imeandikwa na Godfrey Mushi (HAI), Nebart Msokwa (MBEYA), Pilly Kigome (DAR), Neema Hussein (MPANDA) na Julieth Mkireri (KIBITI)**


## PUBLIC NOTICE

Dear Esteemed Customers,
Equity Bank Tanzania is a commercial bank with a presence in six countries in East Africa: Kenya, Uganda, Tanzania, DRC Congo, Rwanda, and Ethiopia. In Tanzania, we operate 15 branches, over 3000 agents, and 21 ATMs, offering an array of banking services, including mobile money services through the Equity Mobile App and USSD.

This is to inform our customers that the bank has made some changes on the Bank charges as per the below:

| Service | Tariff |
|---|---|
| Online Declined Visa card Transaction (Local) | 2 USD |
| Online Declined Visa card Transaction (International) | 2 USD |
| ATM cash withdrawal outside Tanzania | TZS 12,000 + 15% Mark-up of FX rate |
| International POS (Point of Sale) and e-Commerce Transactions | 15% Mark-up of FX rate |

**For more information:**

Please call **+255 768 985 500 / +255 768 985 555**
or through email **infotz@equitybank.co.tz**

EQUITY


## Lori la mafuta laanguka, wananchi wachota mafuta

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

AJALI za barabarani katika Mkoa wa Pwani zimeendelea kuwa tishio licha ya elimu na adhabu zinazoendelea kutolewa kwa wanaokiuka sheria.

Ndani ya siku 18 kuanzia Machi 28, mwaka huu, ajali nne zimetokea katika mkoa huo na kugharimu maisha ya watu na kuharibu vyombo vya usafiri walivyokuwa wanatumia.

Kukiwa na hali hiyo, ajali zinapotokea baadhi ya watu wamekuwa wakiwaibia waathirika badala ya kuzilinda mali zao na kusaidia kuokoa maisha yao.

Licha ya kupata somo kutokana na madhara yaliyotokea kwa wananchi wanaochota mafuta pindi malori ya mafuta yalipoanguka katika maeneo mbalimbali, vitendo hivyo vinaendelea huku hali duni za kiuchumi ikitajwa kuwa chanzo cha baa hilo.

Jana saa sita mchana, kulitokea ajali katika eneo la Miyomboni, Kata ya Misugusugu, wilayani Kibaha, mkoani Pwani ambako gari la mafuta liliacha njia na kupinduka.

Wananchi wa maeneo ya karibu na eneo la tukio walikusanyika wakiwa na vyombo mbalimbali vya kuchotea mafuta na kuondoka nayo badala ya kusaidia kuokoa.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Miyomboni ilikotokea ajali hiyo, Salum Nguzo alisema gari hilo lilipofika katika eneo hilo kulikuwa na lori lingine ambalo liliingia kwenye mtaro na kuacha tela lake nyuma.

"Kwahiyo, huyu mwenye lori alipunguza mwendo ili asubiri gari za upande wa kushoto zipite kisha naye apite, alizidi sana upande wa kushoto na hali ya mvua ilivyokuwapo, gari likaingia kwenye mtaro, hata alivyojitahidi kurudisha likaanguka taratibu kwenye mtaro," alisimulia mwenyekiti huyo. Nguzo alisema baada ya gari hilo kupinduka, wananchi walisogea na kuanza kuchota mafuta mpaka pale walipofika askari na kuwazuia kuendelea kufanya hivyo na ukafungwa utepe kuzuia wananchi kuendelea kuchota mafuta.

Alisema kitendo cha wananchi kuchota mafuta gari linapodondoka kinatokana na hali duni za maisha bila kujali uhai wao. "Wananchi wanachoangalia ni kupata fedha tu, hawajihurumii, changamoto za maisha zinafanya kuwa hivi kwani wakiyapata wanakwenda kuuza ili wapate kipato," alisema.

Pamoja na kukamatwa kwa waliohusika kuchota mafuta, kiongozi huyo alishauri msako wa nyumba kwa nyumba ufanyike ili kukomesha tabia hiyo na madhara ambayo yanaweza kutokea.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Pius Lutumo alisema tukio hilo lilitokea jana saa sita mchana, lori hilo la mafuta lenye namba za usajili T 964 DLH likiwa linatokea jijini Dar es Salam kuelekea Chalinze.

Kamanda Lutumo alisema hakuna madhara kwa binadamu yaliyotokea katika tukio hilo na kwamba watu sita wanekamatwa kutokana na kitendo cha kuchota mafuta baada ya gari hilo kupinduka.

# Mwinyi: Kero zinaendelea katafutiwa ufumbuzi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR



RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi (pichani), amesema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zimeendelea kuchukua hatua madhubuti za kuzitafutia ufumbuzi changamoto zote zinazojitokeza katika utekelezaji wa masuala ya Muungano.

Aliyasema hayo jana kwenye viwanja vya maonesho ya biashara Nyamanzi, nje ya mji wa Zanzibar wakati wa uzinduzi wa sherehe za maadhimisho ya miaka 60 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Alisema kwa nyakati mbalimbali juhudi zikichukuliwa na serikali zote mbili ambazo ni pamoja na kuundwa kwa tume na kamati kwa ajili ya kushughulikia hoja za Muungano na miongoni mwa tume na kamati hizo ni Kamati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kushughulikia masuala ya Muungano iliyoundwa mwaka 2006.

Alisema kuanzia mwaka 2006 hadi mwaka huu wa 2024, hoja 25 zilipokewa na kujadiliwa na kati ya hoja hizo, 22 zimepatiwa ufumbuzi na kuondolewa kwenye orodha ya hoja za Muungano.

Alisema, hoja zilizobaki zipo katika hatua mbalimbali za kupatiwa ufumbuzi na imani yake kuwa, kwa utashi na dhamira ya dhati ya serikali za pande zote mbili, zilizobaki zitapatiwa ufumbuzi.

Aidha, alisema katika kipindi cha 2021 hadi 2024 hoja 15 zimepatiwa ufumbuzi kati ya hoja 18 zilizokuwapo na utatuzi wa changamoto za Muungano, umeongeza imani ya Watanzania kwa serikali na hivyo kuimarisha, kudumisha amani ya muda mrefu na utulivu wa Tanzania ambao ni tunu muhimu na fahari ya nchi.

"Nawahakikishia wananchi wote wa Tanzania, kwamba serikali zote mbili zitaendelea kuchukua hatua ili nchi yetu iendelee kupiga hatua za maendeleo na ibaki kuwa nchi ya amani na utulivu."

Alisema wananchi wa Tanzania wana matumaini makubwa na Muungano huo, pamoja na taasisi zote zinazohusika katika kuufanya uendelee kudumu na kuimarika na kwamba ni vyema kutafakari kwa kina historia yake, dhamira ya waasisi wake na manufaa yake.

Kadhalika, Watanzania wanaposherehekea miaka 60 ya Muungano wa Tanzania, wana wajibu wa kujipongeza kwa mafanikio makubwa ambayo nchi imeyafikia katika nyanja zote za maendeleo kisiasa, kiuchumi na huduma za jamii.

"Katika kipindi hiki cha miaka 60, Tanzania imeendelea kubaki katika historia na mfano bora wa kudumisha Muungano barani Afrika na duniani kote. Muungano wetu umeipa heshima kubwa nchi yetu katika Jumuiya ya Kimataifa," alisema Dk. Mwinyi.

Alisema hiyo imetokana na misingi thabiti ya umoja, amani na mshikamano iliyoasisiwa na viongozi ambao ni Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Marehemu Mzee Abeid Amani Karume pamoja na viongozi wenzao waasisi wa Muungano.

Aidha, dhamira yao ya dhati na maono ya waasisi hao, kumewezesha kupata hatua kubwa ya mafanikio yaliyofikiwa katika kudumisha na kuimarisha Muungano wa Tanzania.

"Tunafurahia kuona umoja wa Watanzania unazidi kuimarika, ushirikiano baina yetu katika shughuli mbali mbali unaongezeka na amani ya nchi yetu inaendelea kudumu," alisema.

Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, aliwashukuru Rais Dk. Mwinyi na Dk. Samia, wanavyoliongoza taifa kwa misingi ya kusimamia Muungano.

Alisema, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar na Ofisi ya Muungano na Mazingira ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zinawajibu wa kuielewesha jamii juu ya historia ya Muungano kwa vizazi vilivyopo.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira Dk. Selemani Saidi Jafo, alisema historia ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeundwa na sababu nyingi hadi kufikia kusainiwa kwa hati ya Muungano mwaka 1964 chini ya waasisi wake Hayati baba wa Taifa Julius Nyerere na Marehemu Mzee Abeid Amani Karume.

Akitaja baadhi ya sababu hizo zikiwemo urafiki na udugu wa damu wa wananchi wa pande mbili za Muungano, lugha ya Kiswahili iliyowaunganisha watu wa pande hizo, pamoja vyama vya ukombozi vya TANU na ASSP, Waziri Jafo alisema vilitoa mchango mkubwa kwenye Muungano huo.

Alisema katika kusherehekea maadhimisho ya miaka 60 ya Muungano wa Tanzania, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar wanatarajia kuzindua kitabu maalum kinachoeleza historia ya Muungano wa Tanzania kwa ajili ya kufundishiwa shule za sekondari nchi nzima.

Uzinduzi wa sherehe za miaka 60 ya Muungano wa Tanzania na ufunguzi wa Maonesho maalum ya Taasisi za Muungano chini ya kaulimbiu, "Tumeshikamana na Tumeimarika kwa Maendeleo ya Taifa Letu", unaashiria kuanza rasmi kwa shughuli mbalimbali za kijamii ikiwamo upandaji wa miti, usafi wa mazingira na ushiriki wa wananchi na viongozi kwenye matukio ya uzinduzi wa miradi ya maendeleo na uwekaji wa mawe ya msingi kwa maeneo mbalimbali ya Tanzania.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA KILIMO**
**WAKALA WA TAIFA WA HIFADHI YA CHAKULA**
Kizota Viwandani Area | S.L.P 1050 Dodoma | Simu: +255(0)26 2963953 | Fax:+255(0)26 2963950
Barua pepe: info@nfra.go.tz | Tovuti: www.nfra.go.tz

NFRA

## TANGAZO KWA UMMA

### UFAFANUZI KUHUSU UTUMIAJI WA MIKATABA YA MBELE YA UNUNUZI WA MAHINDI NA MPUNGA NA KUANZA KUTUMIA MIZANI ZA KIDIGITALI WAKATI WA UNUNUZI WA NAFAKA

Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) ni Taasisi ya Serikali chini ya Wizara ya Kilimo. NFRA imeanzishwa chini ya Sheria ya Wakala za Serikali Na. 30 ya mwaka 1997 kwa madhumuni ya kuhakikisha usalama wa chakula Nchini. Katika kutekeleza moja ya majukumu yake, NFRA hununua nafaka kwa ajili ya Akiba ya Taifa ya chakula. NFRA inatarajia kununua Mahindi Meupe na Mpunga katika msimu wa ununuzi wa mwaka 2024/2025, kuanzia tarehe 1 Julai, 2024. Ununuzi utafanyika kupitia kanda nane za Wakala ambazo ni Arusha, Dodoma, Kipawa (Dar es Salaam), Makambako, Songwe, Shinyanga, Songea na Sumbawanga.

Kipindi cha **tarehe 26 Machi, 2024** hadi **tarehe 03 Aprili, 2024,** NFRA ilitoa Matangazo ya kununua mahindi na mpunga kwa utaratibu wa mikataba ya mbele kutoka kwa **Wakulima na Wafanyabiashara wakubwa.** Sambamba na Tangazo hilo, NFRA inaujulisha Umma kwamba utaratibu wa kununua nafaka kupitia vituo vya ununuzi katika maeneo mbalimbali Nchini unaendelea kutumika wakati wa msimu wa ununuzi wa nafaka. Utaratibu huu unawezesha **Wakulima wote wadogo** kuweza kuuza nafaka zao moja kwa moja kwa NFRA bila kuwa na mikataba. Msimu wa 2023/2024 NFRA ilifungua vituo vya ununuzi sabini na saba (77) na inatarajia kufungua vituo zaidi vya ununuzi kwa msimu wa 2024/2025 katika maeneo mbalimbali Nchini.

Aidha, ili kuongeza uwazi katika vipimo wakati wa utekelezaji wa zoezi la ununuzi wa nafaka, NFRA inaujulisha Umma kwamba kuanzia msimu ujao wa ununuzi wa nafaka (2024/2025), itatumia mizani za kidigitali (digital weighing scales) kupima uzito wakati wa kununua nafaka kutoka kwa Wakulima. Vituo vyote vitakavyofunguliwa vitatumia mizani hiyo ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa kazi ya ununuzi wa nafaka na kupunguza malalamiko wakati wa upimaji wa nafaka zinazoletwa kuuzwa kupitia vituo vya NFRA.

Baada ya ufafanuzi wa hapo juu, Wakulima wote mnakaribishwa kuuza nafaka NFRA msimu wa ununuzi utakapoanza.

**Imetolewa na:**

**Afisa Mtendaji Mkuu,**
**Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula,**
**Tarehe 08 Aprili, 2024.**
**Simu Namba: +255 (0) 26 2963953**
**Baruapepe: info@nfra.go.tz**



Mstahiki Meya wa Jiji la Dar es Salaam, Omary Kumbilamoto, akishiriki katika zoezi la kugawa chakula kwa waathirika wa mafuriko wilayani Rufiji, mkoani Pwani juzi. Jumla ya vyakula vyenye thamani ya sh. milioni 50 na ng'ombe watano walikabidhiwa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Vigogo kuwekwa 'kitanzini'

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMA si leo basi kesho ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa Mwaka 2022/23 zitawasilishwa bungeni kwa mujibu wa sheria.

Mkutano wa Bunge la Bajeti leo unaingia katika juma la tatu na Ibara ya 143 ya Katiba ya nchi (1977) inaelekeza kuwa Rais baada ya kukabidhiwa ripoti za CAG, anapaswa kuziwasilishe bungeni kupitia wasaidizi wake ndani ya siku saba tangu kuanza kwa mkutano unaofuata wa Bunge (siku za sikukuu na mwishoni mwa wiki hazihesabiki).

Rais Samia Suluhu Hassan alipokea ripoti ya CAG Machi 28, mwaka huu. Mkutano wa Bunge ulianza Aprili 2, 2024, hivyo kutokana na siku za sikukuu na mwisho wa wiki kutohesabika, zimesalia siku mbili kati ya saba kuwasilisha ripoti hizo bungeni kukidhi matakwa ya kikatiba.

Kuwasilishwa ripoti bungeni na hivyo kuwa wazi kwa umma, kunatarajiwa kuwaweka 'kitanzini' baadhi ya watendaji wa serikali ambao CAG Charles Kichere ameweka wazi kwamba taasisi zao zina dosari kiutendaji ikiwamo matumizi mabaya ya fedha za umma.

Hao ni pamoja na vigogo wa taasisi kama vile Bohari ya Dawa (MSD), Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka jijini Dar es Salama, Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), Bodi ya Utalii Tanzania (TTB) na watendaji wa halmashauri.

Katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, kwa mfano, CAG Kichere alidokeza katika wasilisho lake kwa Rais Samia Machi 28, mwaka huu kuwa amebaini bado kuna shida ya ulaji wa 'fedha mbichi' (kutumia fedha za makusanyo kabla ya kuziwasilisha Mfuko Mkuu wa Serikali), udhaifu katika ukusanyaji mapato na kutotenga fedha kwa ajili ya makundi maalum.

Vigogo wengine wanaotarajiwa kuwekwa 'kitanzini' na CAG ni wa mashirika ambayo yanatajwa kujiendesha kwa hasara. Hayo ni pamoja na Shirika la Posta Tanzania, Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL), Shirika la Mawasiliano (TTCL), Shirika la Reli Tanzania (TRC) na Kampuni ya Uwekezaji ya TANOIL.

Ripoti za CAG zitakazowasilishwa bungeni ni: Ripoti Kuu ya Ukaguzi; Ukaguzi wa Hesabu za Serikali Kuu; Ukaguzi wa Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa; Ukaguzi wa Hesabu za Mashirika ya Umma; Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo; Ukaguzi wa Mifumo ya Tehama na Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi.

Pia kuna ripoti za ukaguzi wa ufanisi katika maeneo maalum 14, mojawapo ni hali ya utoaji huduma za ugonjwa wa akili nchini.

Baada ya kuwasilishwa bungeni na mawaziri husika, ripoti za CAG zitakabidhiwa kwa kamati za Bunge zenye mamlaka ya kuifanyia uchambuzi.

Pamoja na hayo, juma hili wabunge watapata majibu ya hoja zilizoibuka kwenye mjadala wa Mapitio ya Utekelezaji Bajeti ya Mwaka 2023/24 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge kwa Mwaka 2024/25.

Hoja hizo ni pamoja na sakata la kikokotoo cha mafao ya wastaafu, tishio la kufilisika Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), ugumu wa upatikanaji mikopo ya elimu ya juu na nishati safi ya kupikia vijijini.

Nyingine ni kilio dhidi ya wanyama hatari kwa binadamu, hasa tembo na mamba, kukithiri kwa mikopo kausha damu, matumizi ya shisha, madeni ya askari magereza na utitiri tozo kwenye sekta ya uvuvi.

Baada ya kuhitimishwa mjadala huo, kutawasilishwa hoja ya makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwa Mwaka 2024/25 itakayojadiliwa kwa siku tatu na kufuatiwa na Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora itakayojadiliwa kwa siku moja.

## Shekhe: Ole wenu mnaodhulumu yatima

**Na Julieth Mkireri,** BAGAMOYO

SHEKHE wa Mkoa wa Pwani, Hamis Mtupa ameonya watu wenye tabia ya kudhulumu mali za yatima, akiwataka kuacha mara moja kwa kuwa dhuluma hiyo ni hatari kwa maisha yao ya baadaye.

Alionya hayo mwishoni mwa wiki akiwa mjini Bagamoyo alikoshiriki dhifa kwa ajili ya watoto yatima, wajane na wazee iliyoandaliwa na Taasisi ya SHAKIBA Islamic Foundation ya Bagamoyo.

Alisema baadhi ya watu wamekuwa na tabia ya kunyanyasa na kudhulumu mali yatima ambao wameachiwa mali na wazazi wao na kuzitumia huku watoto hao wakiendelea kupata tabu.

"Watu wanaokula au kujinufaisha na mali za yatima ni sawa na kula kaa la moto kwa kulitia tumboni, moto huo utawachoma baadaye na kila watakalolifanya haliwezi kufanikiwa," alisema Shekhe Mtupa.

Mwenyekiti wa SHAKIBA, AbdulSharifu Zahoro alisema lengo la kuanzisha taasisi hiyo ni kusaidia watu mbalimbali wenye mahitaji, wakiwamo wajane, yatima na wazee.

Zahoro alisema tayari wameanzisha kituo cha kulea yatima; kwa sasa wanao 124 huku 24 wakiwa shuleni.

Mkurugenzi wa Firdaus Centre, Kituo cha Kulea Yatima cha Kongowe Kipala Mpakani, Dk. Shekhe Sharifu Firdaus alisema yatima wanakumbana na vikwazo vingi baada ya kufiwa na wazazi wao.

Mwenyekiti Idara ya Wanawake ya SHAKIBA, Jamila Suleiman alisema wanapigania haki za wanawake na dini haitaki wanawake wanyimwe haki zao, akisisitiza vipigo huondoa upendo na kusababisha visasi.

Mratibu wa SHAKIBA Taifa, Dk. Fakhad Mtonga alisema lengo lingine la kuanzishwa taasisi hiyo ni kusaidia jamii kwenye masuala mbalimbali, ikiwa ni pamoja na afya, elimu, kilimo, uvuvi na elimu ya dini.

Alisema wamekuwa wanatoa elimu ya kukabili vitendo vya ukatili wa jinsia, kujitambua na kukabili vitendo viovu na wanatarajia kuanzisha kituo cha afya ambacho wasiojiweza watatibiwa bila malipo na watu wengine watalipia gharama za matibabu kwa bei nafuu.

PROFESA AHADHARISHA:

# Wakazi Dar kutembea na oksijeni miaka mitano ijayo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

PROFESA wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Julius Nyahongo ametahadharisha kuwa katika miaka mitano ijayo wakazi wa Jiji la Dar es Salaam wataanza kutembea na oksijeni mfukoni kutokana na ongezeko la joto linalosababishwa na ukataji miti ovyo.

Alitoa angalizo hilo mwishoni mwa wiki wakati wa mdahalo wa kumbukizi ya miaka 102 tangu kuzaliwa kwa Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere uliofanyika jijini hapa kwa uratibu na Taasisi ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere.

Prof. Nyahongo alisema mazingira kwa sasa ni mabaya na alishafika ofisini kwa Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango kumweleza kwamba ili kumuenzi Mwalimu Nyerere, kinachotakiwa ni kutunza kwa mazingira.

"Makandarasi wanapotaka kujenga jengo, wanafyeka eneo kubwa mno. Wakiulizwa wanasema wanapima, wanasahau hiyo miti imehangaika sana kukua. Ninaomba Makamu wa Rais (Dk. Mpango) waambie makandarasi wote wa Tanzania wanapotaka kujenga wakumbuke ile miti imeota pale kwa shida, wakate sehemu ndogo wanayojenga pekee yake.

"Pale Dar es Salaam miaka mitano ijayo watu wataanza kutembea na oksijeni mfukoni, pale Kisutu wamejenga maghorofa mengi na chini wameweka paving (vipande vya matofali) ili maji yasiende chini yatelemke kwenda bondeni, ndiyo maana kila siku mafuriko watu wanakufa, nchi hii tunajenga vizuri, lakini tunasahau kuacha njia za maji kupita kwenda chini ya ardhi," alisema.

Alisema kwa wakazi wa Jiji la Dar es Salaam, mchana watakosa oksijeni ya kuvuta na vibaka wa miaka 10 ijayo hawataiba simu, wataiba vitu vya kubeba Oksijeni.

"Watu watatembea na oksijeni na hata hapa mjini kwako, pale Dar es Salaam twende tubomoe paving, tuoteshe miti ili kunusuru hali ya hewa safi na pia miji ipangwe kisayansi," alishauri.

Alisema oksijeni inatengenezwa na miti na kwa sasa watu wa mijini wanataka kila sehemu wajenge bila kutenga eneo la kupanda miti. "Utakuta watu wamelala ofisini mchana kwa sababu hakuna oksijeni, kuna kabonidaioksaidi nyingi, tunaomba miji yetu tuanze kupanga kisayansi na wanasayansi ni sisi, niite nitakueleza," alisema.

Awali akizungumzia mazingira, Mkuu wa Shule ya Uongozi ya Mwalimu Nyerere, Prof. Marcellina Chijoriga, alisema Mwalimu Nyerere wakati wa uongozi wake alihimiza utunzaji mazingira na wanyamapori kwa faida ya vizazi vya sasa na vijavyo.

"Tusipotunza mazingira, hii hewa tunayovuta hatutaipata, misitu inatunza baionuai inayoleta maji, kila mtu anaona umuhimu wa maji na Baba wa Taifa wakati ule alisema maji ni uhai, tutunze mazingira kwa ajili ya uhai," alisema.

Akitoa pongezi maalum za taasisi hiyo katika uongozi wa Rais Samia na miaka 60 ya Muungano, Mbunge wa Kilosa, Prof. Palamagamba Kabudi, alisema kitabu cha Hayati Mwalimu Nyerere cha Uhuru wa Wanamke alichoakiandika mwaka 1944 akiwa na miaka 22, kinaakisi uongozi mahiri na matendo makubwa ya Rais Samia.

Hivyo, alipongeza Rais Samia kutokana na kuenzi, kuimarisha na kudumisha Muungano na kuendeleza misingi iliyowekwa na Mwalimu Nyerere ambayo ni umoja wa taifa, siasa safi na uongozi bora, utashi wa kisiasa wa kuendeleza na kuthamini Muungano.

# Ufungaji wa kamera gerezani waanza

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

SERIKALI imeanza kufunga kamera maalum (CCTV) katika maeneo ya magereza ili kuimarisha usalama na ulinzi, pia kwenda na sayansi na teknolojia katika utoaji na ufuatiliaji huduma kwa wadau mbalimbali wanaoshirikiana nao kama Jeshi la Polisi na Mahakama.

Naibu Kamishna wa Jeshi la Magereza, Jeremia Katungu alibainisha hayo jana wakati wa ziara ya Naibu Waziri, Daniel Sillo, ambaye alihudhuria pia mkutano wa uongozi wa juu wa jeshi hilo uliohusisha maofisa, askari na watumishi raia.

"Tunashukuru serikali kwa kuliwezesha jeshi katika maeneo mbalimbali ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji majukumu yake.

Baadhi ya maeneo hayo ni ununuzi wa vifaa vya ulinzi na usalama katika maeneo yanayozunguka magereza," alisema.

Alibainisha kuwa kwa sasa usimikaji kamera hizo unaendelea katika maeneo ya magereza ya Maweni, mkoani Tanga; Karanga, mkoani Kilimanjaro; Luanda, mkoani Mbeya na Tabora.

Naibu Kamishna Katungu alisema maeneo yaliyoboreshwa na serikali ni pamoja na kuwapatia vyombo vya usafiri, ajira, upandishwaji vyeo kwa askari na maofisa ambapo hadi sasa jumla ya ajira 662 ziko katika mchakato wa usaili huku upandishwaji vyeo ukifanywa kwa askari na maofisa 4,111.

Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Sillo, katika kikao hicho aliagiza askari wa Jeshi la Magereza kuwa na nidhamu katika utendaji wao wa kazi ili kujiepusha na tuhuma mbalimbali ambazo zitachafua jeshi.

Alipongeza serikali kwa kutoa kipaumbele kwa jeshi hilo na vyombo vya ulinzi na usalama kwa kuhakikisha wanapata mahitaji yote ya msingi.

"Sifa kubwa ya askari ni nidhamu.

Nidhamu hiyo inapaswa kuanzia ndani ya jeshi mpaka nje. Ninawaomba mwendelee kuboresha nidhamu kazini ili kuboresha uhusiano wenu pamoja na viongozi wenu, jueni serikali inawategemea sana katika utoaji huduma.

"Maelekezo yake ni kuwa Tume ya Haki Jinai ilishatoa mapendekezo, sasa yafanyiwe kazi ili kuondoa baadhi ya changamoto ikiwamo msongamano wa wafungwa gerezani," alisema Naibu Waziri.

## CRDB yatangaza ongezeko la asilimia 21 faida baada ya kodi mwaka 2023

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya CRDB imetangaza matokeo ya kifedha ya kuvutia kwa mwaka wa fedha uliomalizika Disemba 31, 2023, ikitangaza ukuaji wa asilimia 21 katika faida baada ya kodi ikiwa ni ongezeko kutoka Sh. bilioni 351 mwaka 2022 hadi kufikia Sh. bilioni 423 mwaka 2023.

Imeelezwa kuwa ukuaji huo wa faida unakwenda sambamba na dhamira ya benki hiyo katika kuongeza thamani ya uwekezaji wa wanahisa wake, ambapo pendekezo la gawio Sh. 50 kwa kila hisa limetolewa na Bodi ya Wakurugenzi, ikifanya jumla ya gawio kuongezeka hadi Sh. bilioni 131, ikiwa ni ukuaji wa asilimia 11. Pendekezo hilo la gawio linategemea uidhinishwaji wa mamlaka za usimamizi.

Imeelezwa na uongozi wa benki hiyo kwamba utendaji wa kipekee wa benki ulichangiwa kwa kiasi kikubwa na ukuaji katika mapato ya fedha zilizofadhiliwa na zisizofadhiliwa. Mapato yaliyofadhiliwa (mapato ya riba) yaliongezeka kwa asilimia 29 kufuatana na ukuaji mizania ya mikopo. Mapato halisi ya riba hata hivyo yalikua kwa kiwango cha chini cha asilimia 19, yakisababishwa na ukuaji gharama za riba kwa asilimia 58 kutokana na kupanda kwa viwango vya riba katika soko la ndani na la kimataifa. Benki ya CRDB na kampuni zake tanzu ziliendelea kurekodi ukuaji wa kuvutia katika mapato yasiyofadhiliwa (mapato ya ada na kamisheni) ambayo yalionesha ukuaji wa asilimia 11 kutokana na matumizi makubwa ya njia za kidijitali. Hiyo inajidhihirisha katika kuimarika kwa mapato kwa kila hisa kwa asilimia 20 kufikia Sh. 161.9.

Kulingana na matokeo ya kifedha yaliyokaguliwa ya benki kwa mwaka 2023 yaliyotolewa, benki pia iliripoti ukuaji mkubwa katika viashiria muhimu vya utendaji. Jumla ya mali iliongezeka kwa asilimia 14 kutoka Sh. trilioni 11.6 hadi Sh. trilioni 13.3. Mikopo na amana za wateja pia zilirekodi ukuaji mkubwa wa asilimia 23 na asilimia nane kufikia Sh. trilioni 8.5 na Sh. trilioni 8.9. Pia, jumla ya fedha za wanahisa zilifikia Sh. trilioni 1.8.

Abdulmajid Nsekela, Mkurugenzi Mtendaji wa Kundi la Benki na Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB alisema utendaji thabiti wa benki ulitokana na utekelezaji mzuri wa mkakati wake wa ukuaji endelevu na mfumo thabiti wa biashara wenye uwezo wa kukabiliana na changamoto za kikanda na kimataifa. Nsekela alisisitiza kuwa utekelezaji mkakati mpya wa kati wa Benki (2023-2027) umekuwa kichocheo muhimu cha kupata utendaji mzuri. "Utekelezaji makini wa mipango yetu ya kimkakati umechangia kwa kiasi kikubwa ukuaji huu wa kipekee," alisema Nsekela na kubainisha kuwa juhudi za benki za kukuza biashara kwa wateja wadogo na wakati zimeshuhudia ukuaji wa asilimia 35 katika mikopo kwa wajasiriamali wadogo wa kati (MSMEs), na maendeleo makubwa katika ujumuishi kifedha katika makundi mbalimbali kama vile vijana, wanawake, kilimo na ufadhili endelevu.

"Hii imepelekea ongezeko kubwa la idadi ya wateja wanaotumia huduma za kidijitali. Ukuaji huu katika matumizi ya mifumo ya kidijitali unaendelea kukuza mchango wa huduma za wateja wadogo na wa kati katika matokeo ya benki kwani mapato kutoka huduma za kidijitali yaliongezeka kwa asilimia 11 kulinganishwa na mwaka 2022, na amana za kundi hilo pia zilikua kwa asilimia 23. Mwaka wa 2023, Benki ya CRDB iliendelea kupanua wigo wa huduma zake kwa kuingia katika soko la Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) na Kuanzisha kampuni ya bima ya, CRDB Insurance Company Ltd nchini.

Fredrick Nshekanabo, Ofisa Mkuu wa Fedha wa Benki ya CRDB, alisema mkazo wa benki katika kuhakikisha usimamizi bora wa mikopo unajidhihirisha katika uwiano wa mikopo chechefu, ukiendelea kubakia katika asilimia 2.8.



Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu (katikati), akipimwa urefu, baada ya kushiriki matembezi ya kilomita tano, yaliyoandaliwa na Shirika la Afya Duniani (WHO), jijini Dar es Salaam juzi, ikiwa ni mwendelezo wa maadhimisho ya Siku ya Afya Duniani, ambayo ilianza Aprili 7, mwaka huu. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

## Wataka hatua dhidi ya udhalilishaji viongozi wanawake kwenye mitandao

**Na Mwandishi Wetu**

JUMUIYA ya Wanahabari wa Mitandao ya Kijamii (JUMIKITA) imelaani udhalilishaji wa viongozi wanawake kwenye mitandao ya kijamii huku ikizitaka taasisi za wanawake kupaza sauti kukemea tabia hiyo ambayo inadhalilisha na kuumiza watu.

Imehimiza vyama vya wanawake kama vile Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), Umoja wa Wanasiasa Wanawake (WCP-Ulingo), Chama cha Wanasheria Wanawake (TAWLA) na wanaharakati binafsi kujitokeza kulaani vitendo hivyo katika kuunganisha nguvu na kusema "hapana" kwa udhalilishaji wanawake.

Mwenyekiti wa JUMIKITA, Shaban Matwebe, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, alisema ili kulinda maadili katika jamii kwa kizazi cha sasa na kijacho, jamii haina budi kujenga msingi mzuri wa kukemea udhalilishaji mitandaoni bila kujali utofauti wa itikadi za kisiasa, dini au kabila la mtu.

"Hivi karibuni kumezuka tabia mpya ya watu badala ya kujadiliana kwa hoja, kutoa mawazo yao au kukosoa serikali kwa mujibu wa katiba yetu, wameanza kutoa matusi mazito kwa Watanzania wenzao, viongozi wao na wakubwa wao katika umri," alisema Matwebe.

Alisema jumuiya hiyo inaomba viongozi wa dini kusimamia maadili kwa waumini wao katika kipindi hiki ambacho maadili yameporomoka katika jamii ili kurejesha jamii katika msingi ya maadili mema na tamaduni za Kitanzania.

Wiki iliyopita, akiwa katika maadhimisho ya kumbukumbu kifo cha Waziri Mkuu wa zamani, Edward Sokoine, Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda alidai anafahamu baadhi ya watu wakiwamo mawaziri ambao wanatuma watu kumtukana Rais Samia Suluhu kwenye mitandao ya kijamii na kuahidi kuwataja leo iwapo wataendelea.

Mwenyekiti wa TAMWA, Joyce Shebe alipotafutwa kuzungumzia jambo hilo, alisema watajadiliana na viongozi wenzake katika chama hicho na kutoa tamko leo.

"Kwa sasa siwezi kusema kitu, ninawasiliana na bodi na mkurugenzi na leo ni 'weekend' (mwisho wa wiki), pengine kesho tunaweza kuona nini tufanye," alisema.

Katika akaunti yake ya Facebook, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba jana alionya watu wenye nia ovu ya kuchafua serikali ya Rais Samia hasa katika kipindi hiki cha kuelekea Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu wa mwakani na kuahidi kupambana nao.

"Tulijua kuwa kutakuwapo njama za kukuchafua, sana mwaka 2024 na 2025, tunajua kwenye mikakati yao bado watakuja na mengine ya uongo hivihivi, hatutakubali kuyumbishwa, tutapambana na wanaotumwa na wanaowatuma," alisema katika ujumbe wake huo.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Kesi hizi za usajili kila mara zinaharibu taswira ya soka

**IMEKUWA** ni kama kawaida sasa kila baada ya miezi michache kusikia klabu ya Tanzania imefungiwa na Shirikisho la Kimataifa la Mpira wa Miguu (FIFA), kwa kushindwa kumlipa mchezaji, kocha, kukiuka taratibu na kanuni za uhamisho, au ikipewa siku kadhaa iwe imemalizana nao.

Cha kushangaza ni kwamba unaweza kuona klabu inafungiwa kusajili leo, halafu miezi michache tu, inakuja barua nyingine kutoka FIFA, ikiifungia tena timu ile ile kwa mchezaji mwingine, wakati hata bado haijamalizana na mchezaji wa kwanza, mara myingine inaibuka tena.

Ni hivi majuzi tu, Klabu ya Yanga imefungiwa kufanya usajili wa wachezaji wa ndani ya nje kutokana na kesi kama hizo kwa kukiuka kanuni ya za Shirikisho la Kimataifa la Mpira wa Miguu, FIFA.

TFF, nayo ikapigilia nyundo, nayo ikaifungia Yanga kufanya usajili kwa wachezaji wa ndani.

Sababu iliyotolewa ni kwamba imekiuka kile kilichoelezwa ni 'Annexe 3', ya Kanuni ya Uhamisho wa Wachezaji (RSTP) ya shirikisho hilo, ambapo haikuingiza uthibitisho wa malipo ya uhamisho wa mchezaji husika ambaye hakutajwa na TFF katika Mfumo wa Usajili (TMS), licha ya kukumbushwa kufanya hivyo.

Inawezekana barua ya FIFA iliyoandikwa kwa TFF imeeleza kila kitu, lakini hadi sasa haijajulikana ni mchezaji gani ambaye alisajiliwa na uthibitisho wa malipo ya uhamisho haikuthibishwa.

Kwa mujibu wa barua hiyo, Na suala kufikisha kwenye Sekretarieti ya Kamati ya Nidhamu ya FIFA, ina maana kuna adhabu nyingine zaidi itatolewa? Nadhani haya yote mashabiki wa soka wanahitaji kupata majibu ili suala likae sawa, kwa sababu si tu limewachanganya sana wanachama na mashabiki wa Yanga, pia limewashtua.

Kuna kipengele kinachosomeka kuwa Yanga inatakiwa kutekeleza matakwa hayo kikanuni na kuwasilisha taarifa kwa Sekretarieti ya Kamati ya Nidhamu ya FIFA ambapo suala hilo limefikishwa kwa ajili ya hatua zaidi.

Kwa hapa Tanzania, japo Yanga imekuwa mara kwa mara ina mizozo, lakini klabu nyingi nchini zimekuwa na matatizo kwenye uhamisho, na kuachana na wachezaji na makocha wao kwa usalama bila kudaiana.

Hili limekuwa likilipaka matope nchi yetu na Ligi ya Tanzania ambayo kwa sasa ni ya sita kwa ubora Afrika.

Hali hii inapaswa kuepukwa na kupigwa vita vikali kwani ikiendelea klabu za Tanzania zitakosa uaminifu na kutowapata tena wachezaji bora wa kigeni ambao watakuwa wanaogopa kutotekelezewa matakwa yao, na hata mikataba yao kuvunjwa kiholela na kulazimika kukimbilia FIFA.

Ikumbukwe wachezaji hawa wa kigeni ndiyo wanachangia kwa kiasi kikubwa kulipaisha soka la Tanzania kiasi cha kufanya vema kwa klabu zetu kimataifa.

Tunawashauri viongozi wa klabu za soka nchi kuwa makini sana kwenye mikataba ya makocha wachezaji, uhamisho na vitu vingine vinavyofanana na hivyo, ikiwamo hata kufanya udanganyifu wa nyaraka kwenye mitandao ya uhamisho ya TMS, vinginevyo ipo siku wanaweza kujikuta wanaziingiza klabu zao na hata nchi kwenye matatizo makubwa.

FIFA huwa hawaangalii ukubwa wa timu, hata klabu kubwa barani Ulaya zimekuwa zikipata adhabu, kwa mantiki hiyo ukubwa na sifa ya Tanzania na siasa zetu za mpira wa haziwezi kufanya kazi mpaka huko, zikasamehewa au busara ikatumika.

Tunaamini ushauri huu utafanyiwa kazi kwa mustakabali mpana wa soka la nchini yetu ambalo kwa sasa limepiga hatua kubwa, hivyo hatutarajii kuona linajirudi tena kwa sababu kama hizo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

## Simba tengenezeni upya kikosi chenu, kimechoka, hakina ari

Na Adam Fungamwango

**TANGU** msimu uliopita kikosi cha Simba kilionekana kuwa kimechoka, kinahitaji kufanyiwa marekebisho makubwa.

Matokeo yake kilichofanyika ni kusajili wachezaji ambao walionekana ni kama kuja kuongeza upana tu wa kikosi na wala si wa kuingia moja kwa moja.

Viongozi wa Simba wakaendelea kuamini kuwa kina John Bocco, Mzamiru Yassin, Luis Miquissone, Aishi Manula, Shomai Kapombe, Mohamed Hussein 'Tshabalala', na wenzao wataendelea kuibeba Simba.

Kilichotokea wengi wa wachezaji wao wamechoka. Viwango vyao vimeporomoka na hala kingine cha kuongeza kwenye uwezo walionao.

Waliosajiliwa nao asilimia kubwa hawakuingia moja kwa moja kwenye kikosi, badala yake wengi wamekuwa ni wa benchi, na wanaoaza wameshindwa kuibeba timu kama ilivyokuwa kina Bocco zamani.

Kinachotokea Simba ni kwamba viongozi walishindwa kutambua alama za nyakati. Wakashindwa kusikia kengele ya hatari. Wangefanya hivyo wala leo timu hiyo isingekuwa kama ilivyo sasa.

Simba imekosa mvuto, na hata klabu inazocheza nazo haziiogopi kama ilivyokuwa zamani kwa sababu si tishio tena.

Juzi, baada ya sare ya bao 1-1 dhidi ya Ihefu, Kocha Mkuu, Abdelhak Benchikha, alikaa peke yake benchini kwa zaidi ya dakika 10, akiwa na huzuni kubwa baada ya kushuhudia kitu ambacho hakukitegemea kwa wachezaji wake.

Hiki kinachotokea Simba kwa sasa hakijaja kwa bahati mbaya, bali ni ukosefu wa uwajibikaji kwa viongozi. Ni kitu ilibidi wakifanye?

Baada ya kumalizika kwa ligi ya msimu juzi, wachezaji wengi wa Simba walionekana wamechoka kwa viwango vyao kushuka, kucheza mechi nyingi bila kupumzika, umri na pia tayari wengi walikuwa na mafanikio ya kutwaa ubingwa mara nne, Kombe la FA, pamoja na robo fainali tatu za Ligi ya Mabingwa. Hiyo ilitosha kuanza kutengeneza Simba mpya.

Ilitakiwa kusajili wachezaji wengine ambao wataingia moja kwa moja kwenye kikosi na kuwaweka benchi wale waliopo, na si wa kuja kusubiri.

Badala yake kina Bocco ndiyo wakaendelea kuwa tegemeo hadi ligi ilipomalizika.

Bado viongozi wa Simba hawakushtuka ligi ilipomalizika, haikufanya usajili wa maana hata kwa mabeki wa pembeni kina Tshabalala na Kapombe ambao walitakiwa waletewe wachezaji wa kuingia moja kwa moja, na si kina David Kameta na Israel Mwenda ambao wanasubiri.

Tshababa yupo Simba tangu 2014 akitokea Kagera Sugar, Kapombe aliingia Simba 2013, akitokea Polisi Morogoro, pamoja na kwamba alikwenda nje ya nchi na baadaye kurejea akiwa Azam FC na kurejea tena timu yake ya zamani, haiwezekani hadi leo hii akawa ndiyo tegemeo.

Yanga si tu kwamba haina kina Juma Abdul na kina Kelvin Yondani waliocheza na kina Kapombe na Tshabalala, pia imemuacha hata Djuma Shaaban na kuchukua damu changa, huku Simba ikiendelea na wachezaji wale wale miaka nenda rudi.

Na kwa bahati mbaya sana, karibu misimu mitatu Simba ilikuwa ikisajili wachezaji wakati haina makocha. Viongozi ndiyo walikuwa wanasajili, wakati huo ikiwa ama makocha wameondoka wenyewe, au wametimuliwa na wanaokuja wanakuta usajili umeshafanyika.

Hiki ndicho kilichoimaliza Simba na sasa inatakiwa kufanya usajili mkubwa na wa nguvu.

Kama inataka kurudi kwenye ubora wake, hivyo msimu ujao inabidi itoboke, iwe na fungu kubwa la usajili kuliko wakati mwingine wowote, kwa sababu inavyoonekana wachezaji wake wengi kiasi cha asilimia 80 wamechoka. Hawana nguvu za kuipigania Simba na kwa sasa hawana wanachotafuta, kwani kila kitu wameshapata.

Simba isingefika hapa, lakini hiki kinachoonekana sasa ni alama dhahiri ya kuonyesha kikosi kipya kinahitajika.

Ni wakati sasa wa viongozi kuungana na mwekezaji, pamoja na kocha Benchikha kukaa pamoja na kuangalia ni wachezaji gani wa kusajili kwa ajili ya msimu ujao.

Klabu kama ya Simba, inatakiwa isajili wachezaji wenye uwezo na ubora mkubwa ili kuendana na hadhi yake, kwa sasa ambapo ipo tano bora Afrika, si ya kufanyia majaribio, au yeyote tu anaweza kuichezea.

## HABARI KITAIFA

# Ajitolea eneo lake lijengwe mradi wa maji

**Na Mashaka Mgeta,** BUMBULI

MKAZI wa Kijiji cha Funta katika Halmashauri ya Bumbuli, Wilaya ya Lushoto mkoani Tanga, Amina Idd, ametoa mita za mraba 17 kutoka eneo la makazi yake kwa ajili ya mradi wa maji kwa wakazi wa eneo hilo uliowekewa jiwe la msingi na Mwenge wa Uhuru 2024 jana.

Hatua hiyo ni kukabiliana na ukosefu wa eneo uliosababisha Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira (RUWASA) Wilaya ya Lushoto, kupata changamoto ya kupata mahali panapofaa kwa ajili ya ujenzi wa tangi lenye ukubwa wa lita za ujazo 120,000, ili litumike kutoa huduma ya maji kwa wakazi zaidi ya 4,000 wa kijiji hicho na maeneo ya jirani.

Mradi huo ulifunguliwa jana na Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru 2024, Godfrey Mnzawa wenye ujumbe unaosema, 'Tunza Mazingira na Shiriki Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa Ujenzi wa Taifa Endelevu'.


"Niliwaona RUWASA wakihangaika kutafuta eneo la kujenga mradi wao huu, waliponifuata na kutokana na kero ya maji iliyokuwapo awali, nikaona hakuna sababu ya kushindwa kutoa sehemu ya kiwanja changu hiki kidogo, itumike kwa mradi wa maji wenye maslahi kwa watu wengi zaidi," alisema Amina.

Kwa mujibu wa Amina na uthibitisho wa uongozi wa RUWASA wilayani Lushoto, eneo hilo limetolewa bure, na kwa kutambua utayari wake huo, aliunganishiwa huduma ya maji bure.

Faidha Adam mkazi wa kijiji hicho, amesema ukosefu wa maji uliwasababishia kadhia nyingi ikiwamo kuharibika kwa mahusiano kwenye ndoa, ikiwamo baadhi ya wanaume kutowaamini wake zao waliotumia muda mrefu kwenda maeneo ya mbali kutafuta maji.

Angela Yusuph wa kijiji hicho amesema, ukosefu wa maji uliwasababishia kero ya kupanda milima ili kuyafikia maeneo yenye vyanzo vya maji, huku wakishindwa kumudu mahitaji ya usafi wa mwili na mazingira.

Meneja wa RUWASA Mkoa wa Tanga, Mhandisi Upendo Lugongo, alisema mradi huo ulioanza kujengwa Agosti 18, 2022 na kutarajiwa kukamilika kwa asilimia 100 Aprili 30, 2024 na umegharimu Sh. milioni 833.




Meneja wa Barrick nchini (Barrick Tanzania Country Manager), Melkiory Ngido (kulia) akikabidhi msaada wa mfano wa hundi yenye thamani ya dola 10,000 kwa Mwenyekiti wa taasisi ya Mwangaza (OMCW), Marshalo Chikoleka uliotolewa na taasisi ya Nos Vies en Partage (NVeP) inayofadhiliwa na Rais na Ofisa Mtendaji Mkuu wa kampuni ya Barrick Gold Corporation, Mark Bristow, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Katikati ni Mtaalamu wa Afya na Lishe kwa watoto wenye utapiamlo kutoka taasisi hiyo, Loyce Njilla. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanafunzi wa sheria waibuka wa 2 uendeshaji kesi mahakama Afrika

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WANAFUNZI watatu wa masomo ya Sheria wa Chuo Kikuu cha Waislamu cha Morogoro (MUM), walioiwakilisha Tanzania kwenye mashindano ya umahiri wa namna ya uendeshaji kesi, wameibuka washindi wa pili Afrika na washindi wa nafasi ya 27 duniani kati ya mataifa 153 yaliyoshiriki nchini Marekani.

Wanafunzi hao ni Mwanahawa Dadi, Ranoan Sadiq Halfan na Elias Komba ambao wametaja changamoto walizokutana nazo licha ya kuibuka na ushindi huo.

Mashindano hayo yalifanyika nchini humo Jiji la Washington DC, kuanzia Machi 31 hadi Aprili 7, mwaka huu.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti baada ya kuwasili nchini, walisema mashindano hayo yalikuwa na ushindani mkubwa ikizingatiwa kuwa mitaala ya sheria ya Tanzania na nchi nyingine imetofautiana.

"Changamoto kubwa tuliyokutana nayo na mataifa ya wenzetu, wanasoma shahada ya sheria kwa muda wa miaka mitano, na nyingine miaka minane na wanapohitimu wanafanikiwa kuwa mwanasheria kamili tofauti na hapa kwetu elimu hii tunaipata wa miaka minne," alisema Mwanahawa.

Alisema ili kuendana na mataifa hayo serikali inapaswa kubadilika ili kutoa wanasheria wabobezi watakaoweza pia kuingia katika masoko ya mataifa mengine.

Alisema, licha ya kubaini tofauti hizo, lakini wamejifunza namna ya kuendesha kesi za kimataifa katika kutatua migogoro ya moja kwa moja baina ya nchi na nchi na kujenga uelewa katika sheria za kimataifa.

Mwanahawa alisema, wanafunzi wenzao wa mataifa waliyokutana kwenye mashindano yao wanasoma kwa vitendo masomo yao ya sheria na kuwatengenezea kuwa na msingi bora kwenye kuifahamu sheria kwa mapana.

Mwanafunzi wa Chuo Kikuu hicho na mshiriki wa mashindano hayo, Halfan ametaja sababu ya kushindwa kupata nafasi ya kwanza ni pamoja na kutokuwa na uwezo wa kupata makocha wa kuwapa mafunzo ya namna ya kwenda kushiriki mashindano hayo.

Alisema pamoja na kutokuwa na walimu wa kuwaelekeza kama nchi nyingine, walionesha uwezo wao mkubwa na kuleta ushindani hasa kwa washiriki kutoka nchi za Afrika.

"Wanafunzi wenzetu kutoka nchi ya Zimbabwe waliokuwa wa kwanza kwa Afrika walituzidi kwa nafasi tano maana sisi tulipambana mpaka mzunguko wa kati ya 12 iliyokuwa inatakiwa kama tungekuwa na makocha kama nchi nyingine nafasi ya kwanza ilikuwa yetu," alisema Halfan.

Mhadhiri wa Chuo Kikuu hicho, anayefundisha masomo ya Sheria, Jadid Suleiman, alisema wanafunzi hao walikwenda kujifunza namna ya kuendesha kesi kwenye Mahakama Bandia kimasomo.

"Hawa wanafunzi wetu watatu walikwenda Marekani kwenye mashindano ya umahiri wa kuendesha mahakama pamoja na kuzifahamu sheria za kimataifa ni maalumu kwa ajili ya kuwapa mafunzi kwa vitendo wanafunzi," alisema Suleiman.

Mhadhiri huyo pia ni Mwanasheria wa Chuo hicho, alisema, mwaka huu ni mara ya pili kwa nchi kupeleka wawakilishi katika mashindano hayo ya kimataifa na mchakato wa kuwapata wawakilishi huwa wa wazi.

**KABWELA** Na Fadhili Mohammed



airtel
A REASON TO IMAGINE

MUONGOZO WA GHARAMA ZA AIRTEL KUANZIA APRILI - JUNI 2024

**LIPIA KADRI UNAVYOTUMIA: KODI IMEJUMUISHWA**

| | | Bei (TSh) |
|---|---|---|
| MITANDAO YOTE | TSH/ sek | 0.50 |
| NDANI YA MTANDAO | TSH/ sek | 0.50 |
| INTANETI | TSH/ Mb | 9.35 |
| SMS ZA NDANI YA NCHI | TSH/ Sms | 8.00 |
| SMS ZA NJE YA NCHI | TSH/ Sms | 215.00 |

**MITANDAO YOTE**

| Muda | Bei(TSh) | Mitandao Yote (Dak) | SMS |
|---|---|---|---|
| Saa 24 | 500 | 30 | 25 |
| Saa 48 | 1,000 | 150 | 25 |
| Siku 7 | 1,500 | 150 | 50 |
| Siku 7 | 2,500 | 300 | 50 |
| Siku 30 | 5,000 | 400 | 100 |
| Siku 30 | 10,000 | 1,200 | 100 |

**BANDO ZA SMS**

| Muda | Bei(TSh) | SMS |
|---|---|---|
| Saa 24 | 200 | 200 |
| Siku 7 | 500 | 1,000 |
| Siku 15 | 1,000 | 5,000 |
| Siku 30 | 1,500 | 10,000 |

**BANDO ZA INTANETI**

| Muda | Bei (TSh) | (MB) |
|---|---|---|
| Saa 24 | 500 | 246 |
| Saa 24 | 1,000 | 492 |
| Siku 3 | 2,000 | 985 |
| Siku 7 | 2,000 | 950 |
| | Smart Junior Investor Account | nil | nil |
| Withdrawal Charges Over the Counter | For Corporate & SME | | |
| | < 15 Million | 2,500 | 1.2% of the amount min 5 |
| | > 15 Million | 1% of the amount max 50,000 | |
| | For Individuals | | |
| | < 10 Million | 8,000 | 1% of the amount min 5 |
| | > 10 Million | 0.12% of the amount max 50,000 | |
| Cheques | Cheque Book Issuance-100 leaves | 67,500 | Equivalent to TZS |
| | Cheque Book Issuance-50 leaves | 34,000 | Equivalent to TZS |
| | Cheque Book Issuance-25 leaves | 34,000 | 15 USD/11 EUR/15 GBP |
| | Counter Cheque Leaf for Corporate & SME | 18,000 | 16 |
| | Counter Cheque Leaf for Individuals | 20,000 | Equivalent to TZS |
| | Stop Payment Local Cheque | 1% of total value with min 50,000 and max 250,000 | Equivalent to TZS |
| Statements | Account Statements on Banking Hall per month | 2,000 per page max 100,000 | Equivalent to TZS |
| | E-Statements (Daily, weekly, Monthly, Quarterly) | Free | Free |
| Standing Order | To other Banks | 5,000+ TISS Charges total 15,000 | 15 |
| | Within the Bank | 5,000 | 5 |
| Telegraphic Transfers | TISS (Incoming transfers) | Free | Free |
| | TISS (Outgoing transfers) | 10,000 | Equivalent to TZS |
| | Outward TT- Customer | Equivalent to FCY | $ 54 via Internet Banking, $ 60 without Internet Banking |
| Other Charges | Account Closure | 50,000 | 50 |
| | Dormant Account Activation | Free | Free |
| TRADE SOLUTIONS | | | |
| Letters of Credit | **Import LC:** | | |
| | Opening L/C | Equivalent to FCY | 1% pq min 250 |
| | Swift Charges | Equivalent to FCY | 60 |
| | L/C acceptance | Equivalent to FCY | 0.10% |
| | **Export LC:** | | |
| | Confirmation charge - unsecured | Equivalent to FCY | 1.2% min 300 per qtr |
| | Document verification | Equivalent to FCY | 150 |
| | Amendments | Equivalent to FCY | 120 flat fee |
| Bonds and Guarantees | Bid Bond | Unsecured 3.6%; Secured 3%; Cash cover 0.6% per qtr | Equivalent to TZS |
| | Performance bonds | Secured 3%; Full cash cover 0.6% per qtr | Equivalent to TZS |
| | Advance payment | Secured 3%; Full cash cover 0.6% per qtr | Equivalent to TZS |
| | Other guarantees | Secured 3%; Full cash cover 0.6% per qtr | Equivalent to TZS |
| DIGITAL BANKING | | | |
| Internet Banking | Subscription | Free | Free |
| | Maintanance Fee | Free | Free |
| | E-Statements | Free | Free |
| | Outward TT | Equivalent to FCY | $54 |
| Mobile Banking | Subscription | Free | n/a |
| | Maintanance Fee | Free | n/a |
| | Balance Enquiry | 200 | n/a |
| | Mini-Statement | 300 | n/a |
| | Full- Statement | 500 | n/a |
| | Fund transfer to other Banks | 10,000 | n/a |
| | Fund transfer to other accounts within BOA | 450 | n/a |
| | Bank to wallet | 1,000 - 49,999 = 2,500<br>50,000 - 99,999 = 3,000<br>100,000 - 199,999 = 3,500<br>200,000 - 499,999 = 5,500<br>500,000 - 1,000,000 = 7,500<br>Above 1,000,000 = 8,500 | n/a |
| | Wallet to Bank | nil | n/a |
| | Forex Rate request | 300 | n/a |
| | Utility Bills Payment | Free | n/a |
| | Airtime Purchase | Free | n/a |
| | SMS Alert | 2500 per Month | n/a |

| TYPE OF CHARGE | PRODUCT | SESAME MAUVE (PURPLE) | SESAME MAUVE (PURPLE) | VISA ELITE | VISA GREEN |
|---|---|---|---|---|---|
| Cards | Joining Fees | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | Card Replacement | 24000 | 24000 | 24000 | 24000 |
| | PIN Re-issue | 7500 | 7500 | 6000 | 6000 |
| | Block card by Bank | 2500 | 2500 | 2000 | 2000 |
| | ATM Cash withdrawal us-on-us | 1300 | 1300 | 1500 | 1500 |
| | ATM Cash withdrawal Domestic us-on-them | 1000-99999=1500<br>100000-400000=1700 | 1000-99999=1500<br>100000-400000=1700 | 3000 | 3000 |
| | ATM Balance enquiry us-on-us | 400 | 400 | 300 | 300 |
| | ATM Balance enquiry Domestic us-on-them | 400 | 400 | 600 | 600 |
| | Cash advance us-on-us | 300 | 300 | 300 | 300 |
| | Cash advance Domestic us-on-them | 1500 | 1500 | 1500 | 1500 |
| | Mini statement us-on-us | 400 | 400 | 600 | 600 |
| | Mini statement BOA network | 400 | 400 | 1800 | 1800 |
| | Failed transactions (Insufficient funds) | 900 | 900 | - | - |

| TYPE OF CHARGE | PRODUCT | CHARGES TZS | CHARGES FCY |
|---|---|---|---|
| Loans | Loan Application Fee | 0.12% of the principal amount minimum TZS 150,000 | Equivalent to TZS |
| | Base/Prime Lending rate | 17% | 8% |

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA VYETI



**JUMA H. SENG'ENGE** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0119/0068** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **KIBAHA SECONDARY SCHOOL** mwaka 2015 na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S0345/0589** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia USAGARA SECONDARY SCHOOL mwaka 2018. Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/ILA/59611/2024**

## KUPOTEA KWA LESENI

**BOSCO BENEDICT CHUWA**
Anatangaza kupotelewa na Leseni ya madini ya Shaba Mwanga –Same yenye namba za usajili **PML. 0766 KLM.**
Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi .
TAARIFA POLISI :
**PHQ/KIL/MOS/7024/2024**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**BOSCO BENEDICT CHUWA**
Anatangaza kupotea kwa kadi ya gari landrover yenye namba za usajili **T 872 DUF.** CHASSIS NO **SALGA2KEXDA120266**
Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi .
TAARIFA YA POLISI:
**PHQ/KIL/MOS/ 7032/2024**

**AFFIDAVIT REGARDING TO THE CONFIRMATION OF DEATH OF THE LATE MASIMA DAUDI PAULO**

**I, HILDA DAUDI PAULO** of Post Office Box 1249 Dodoma Tanzania, Christian. Adult, Female and resident of Dodoma do hereby take OATH and STATE as follows:-

1. That, am the wife of the late **MASIMA DAUDI PAULO**.
2. That, I declare, the said **MASIMA DAUDI PAULO** Passed away since 25th September, 2021.
3. That, the burial of the said **MASIMA DAUDI PAULO** was took place of Mkonze, Dodoma. Tanzania.

**AND I MAKE** this salemn declaration conscientiously believing the same to be true and by virtue of the Oaths and Statutory Declarations Act, Cap R:E 2019.
Declared at Dodoma this 5th day of September 2023

**SWORN** at Dodoma by the said
**HILDA DAUDI PAULO** who is known to me personally/ identified to me by who known to me person ally HURIDA
DEPONENT in my presence this 5th day of September 2020

**BEFORE ME:**
**NAME: FRED PETER KALONGA**
**SIGNATURE................................**
**ADDRESS: P. O. BOX 2556**
**QUALIFICATION: COMMISSIONER FOR OATHS**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JUDITH JOSEPH NGOWI**
anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA IST** yenye usajili namba **T 357 DSY,** CHASSIS NAMBA: **NCP600200046** na ENGINE NAMBA: **2NZ3457052.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA: **852/2024**

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**ELIAH KILANGO MSHANA**
anatangaza kupotea kwa kadi za pikipiki zenye usajili namba **T 182 AVC** na **MC 618 AEZ.** Kwa yeyote atakaeziona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**PHQ/DAR/KIN/58657/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**DIANAROSE BENNY MBOYA**
anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA REGIUS** yenye jina la umiliki **VOLTZON LIMITED** yenye namba ya usajili **T 185 AUA,** CHASSIS NAMBA: **LH1760018931** na ENGINE NAMBA: **5L4898165.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**PHQ/ARU/MER/8723/2024**

**IN THE DISTRICT COURT OF KYELA**
**AT KYELA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 7544/2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE JANETH ANDWELE BULAMBO**

**AND**

**In the matter of Application for letters Administration by MLEKWA HAMAD...............................PETITIONER**

**GENERAL CITATION (RULE 75)**

All persons claiming to have interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 09th day of May, 2024
Dated at kyela this 8th day April, 2024

DISTRICT COURT KYELA TANZANIA
SENIOR RESIDENT MAGISTRATE
KYELA.
DISTRICT RESIDENT MAGISTRATE KYELA

**IN THE DISTRICT COURT OF BUKOBA**
**AT BUKOBA**

**MISC.CIVIL APPLICATION**
**CASE NO 1022/2024**

**GESAP ENGINEERING GROUP LIMITED......APPLICANT**

**VERSUS**

**SONIA ENTERPRISES LIMITED.........1st RESPONDENT**

**MAHAMUD HAJI SWAIBU.......2nd RESPONDENT**

**NOTICE OF MENTION**

**TO; SONIA ENTERPRISES LIMITED AND**
**MAHAMUD HAJI SWAIBU**

**P.O.BOX 447**
**BUKOBA**

**TAKE NOTICE**,that the mentioned case has been set down for mention on the 16th day of APRIL,2024 at 8:30 O'clock in the forenoon,before Hon AW KABUKA-SRM.Your presence is therefore required on the date and the time indicated

Given under my hand and the seal of the court 26th day of March,2024

RESIDENT MAGISTRATE
BUKOBA
SENIOR DISTRICT MAGISTRATE
BUKOBA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA**
**Kituo cha MAKOLE Mkoa DODOMA**

**Shauri la Ndoa Na. 29/2024**

**JINA LA MDAI ........... RUTHISIA DANIEL MASUDI**

**JINA LA MDAIWA .................... JOSEPH ROBERT MANONI**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**KWA**
**JOSEPH ROBERT MANONI**
**0748 700 725**

**Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba**
**MADAI YA TALAKA, MGAWANYO WA MALI NA MATUNZO YA WATOTO**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 15 mwezi 04 mwaka 2024 saa 8:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima keleta shahidi/Mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri hili bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 04 Mwezi 04 Mwaka 2024.

HAKIMU
HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO
MAKOLE - DODOMA

## MNADA WA HADHARA/NOTISI

SEPCO Debt Collections & Auctioneering Co. Ltd tunatangaza notisi ya siku kumi na nne (14) kwa ndugu Biusy Angela Mkumbwa kulipa deni lake la mkopo aliochukua Tujijenge na kushindwa kulipa. Usipolipa ndani ya siku 14 dhamana iliyowekwa itauzwa kufidia au kulipa deni lako.
**Madalali tajwa hapo chini** tunatangazia umma kuwa kutakuwepo na mnada wa hadhara wa kuuza dhamana za wadaiwa kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali hapo chini. Mnada utaendeshwa kwa idhini tuliyopewa na **Tujijenge Tanzania Financial Service Ltd** kama ilivyotangazwa gazetini:-

| Mdaiwa | Dhamana/ Mahali ilipo | Tarehe ya mnada | Dalali |
|---|---|---|---|
| Biusy Angela Mkumbwa | Gari T.420 EDS Toyota **NOAH** -Makumbusho **Yard** | 30/04/2024 | SEPCO Debt Collections & Auctioneering Co. Ltd |
| Afrikana Augustino Mabonya | Kiwanja kipo Fremu 10, Kivule -Ilala | 29/04/2024 | White Miracle Co. Ltd |

**Masharti Mengine:**
Mnada utafanyika mahali dhamana ilipo kuanzia saa nne asubuhi. Mteja atalipa 25% siku ya mnada, 75% atalipa ndani ya siku 14, akishindwa kulipa 25% iliyolipwa hairudishwi na mnada utarudiwa tena.
Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji ni juu ya mnunuzi.

**Mawasiliano piga: SEPCO: 0715683777/ 0716535221**
**Tujijenge (T) Financial Services Ltd: 0718068335**
**White Miracle: 0684937219/0758811276**

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI. TUPIGIE: +255 - 0677 020701

AU

TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO, MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,

PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

Kwa

## HABARI KITAIFA



Moja ya gari la Wakala wa Barabara (TANROADS) likitumika kuondoa magogo makubwa yaliyojaa juu ya daraja la Mto Sanya, linalotenganisha Wilaya za Hai na Siha, mkoa wa Kilimanjaro jana, katika barabara kuu ya Moshi–Arusha iliyofungwa kwa muda na serikali ili kuepusha maafa yasitokee, baada ya mvua kubwa iliyonyesha kusababisha magogo makubwa kujaa juu ya daraja. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Kinana, Nchimbi wafunda wanachama

**Na Waandishi Wetu**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM) Bara, Abdulrahman Kinana amewataka viongozi kutowapendelea wagombea, kutopandikiza watu, na kuacha tabia ya kununuliwa kwa kupokea rushwa, badala yake watende haki kwakuwa kila mmoja ana haki sawa kwenye uchaguzi.

Aidha, Katibu Mkuu wa CCM, Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, amewaahidi wananchi mkoani Katavi kufikisha kilio cha kutaka kujengewa barabara kwa kiwango cha lami kwa Rais Samia Suluhu Hassan ili waondokane na adha ya usafiri.

Amewaahidi wakulima pia CCM kuendelea kuisimamia serikali kuhakikisha mbolea inapatikana kwa wakati na kwa ubora unaotakiwa pamoja na mazao kupata soko la uhakika.

Viongozi hao walitoa kauli hizo kwa nyakati tofauti katika ziara za kuimarisha chama katika mikoa ya Mara na Katavi.

Kinana akizungumza wakati wa kikao maalumu cha Halmashauri ya CCM Serengeti, alisema katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika mwaka huu na mwakani, ili wapate ushindi vizuri ni lazima watende haki na waepuke rushwa kwakuwa ni adui wa haki.

Aidha, alipokea malalamiko ya watu kupotea na kuuawa katika Hifadhi ya Taifa ya Serengeni inayopakana na makazi yao na kueleza kuwa kuishi ni haki ya kikatiba na hakuna mweyue haki ya kukatisha uhai wa mwingine.

"Mtu anakwenda mahali anawatafuta watu anawakusanya, anamtafuta mwenyekiti wa mtaa au kijiji wanakaa kikao kikimalizika wajumbe wanauliza sasa unatuachaje, rushwa ni adui wa haki, inaathiri maendeleo ya taifa letu, anaopokea na anaetoa rushwa anafanya kosa kubwa sana. Mbaya zaidi ni yule anaedai anasema usiponipa tutakutana kwenye chaguzi hiyo sio sawa."

"Mtu anakupa fedha halafu anafanya uongozi wa miaka mitano anakusaidia nini, kwahiyo angalia kiongozi kazi anayoifanyia jamii, usiangalie atakusaidia nini wewe binafsi, kiongozi anayepata kwa rushwa akishapata nafasi hatakujali, kwa sababu nafasi ile akiinunua, hiyo ndio siri, tendeni haki zingatieni Katiba na kanuni ili tupate viongozi wazuri," alisisitiza Kinana.

Alikumbusha kuwa kiongozi mzuri ni yule anayepatikana kwa uadilifu, akieleza kuwa wanawategemea wazee kutoa maoni, kuwaongoza, kuwapatanisha walipoharibikiwa.

Kuhusu mauaji katika eneo la mpaka wa Hifadhi ya Taifa Serengeti ambayo yaliibuliwa na Diwani wa Kata ya Mochochwe, Joseph Mhegete, alisema wananchi wake wamekuwa wakikamatwa, kuuawa na mifugo yao ikikamatwa inataifishwa.

"Watu wamekuwa wakipotea mazingira ya kutatanisha na hatujui mazingira haya kwanini yanatokea kwa sisi tunaoishi pembezoni mwa hifadhi hii," alisema Mhegete.

Mkuu wa Wilaya ya Serengeti, Vicent Mashinji, alikiri kuwapo kwa mgogoro huo, ingawa alisema malalamiko yako kwa pande zote baina ya wananchi na hifadhi.

"Bado tunajitahidi kutoa elimu kwa wananchi wasiingie kwenye hifadhi na maofisa hifadhi wanaojichukulia sheria mkononi tumeagiza wachukuliwe hatua za kinidhamu," alisema Mashinji.

Pia, Kinana alisema kuwa hakuna upande wowote wa kulaumiwa na kwamba iko haja ya viongozi kuendelea kuelimisha wananchi kuheshimu mipaka iliyoko.

"Mkuu wa wilaya ya Serengeti amelifafanua vizuri sana na huwezi kuulaumu upande mmoja peke yake, lakini tuna wajibu wa kuwaelimisha wananchi kuhusu kuheshimu mipaka, jambo moja la msingi hakuna mwenye haki ya kuondoa uhai wa mtu. Hata katika Katiba haki ya kwanza ni kuishi," alisema Kinana.

Pia, serikali hairuhusu maisha ya mwananchi yeyote kupotea na kwa vyombo vya ulinzi na usalama wajibu wake ni kufuata sheria sio kuua.

Alisema serikali imeunda kamati ndogo ambayo itafika mkoani Mara kwa ajili ya kufanya tathmini na hatimaye kutatua changamoto hiyo.

Dk. Nchimbi akizungumza wakati wa kuwaaga wakazi wa Mkoa wa Katavi na kupokewa na wakazi wa Mkoa wa Rukwa, alisema CCM ina wajibu wa kuisimamia serikali ili kuhakikisha inatekeleza ilani na sera zote katika sekta mbalimbali.

Kuhusu ujenzi wa barabara alisema "Nitamwambia Rais, ujenzi wa barabara hii uende kwa kasi ya mbwa koko kwa kasi ya haraka, Mimi mwenyewe nimepita nimejionea hali ilivyo" alisema Nchimbi huku akishangiliwa na wafuasi wa chama hicho waliokuwa wamefurika kupokea salamu zake.

"Kwa kuutazama Mkoa wa Katavi na Rukwa ni miongoni mwa mikoa yenye shughuli za kilimo hivyo katika kuhakikisha serikali inazidi kuweka mazingira rafiki kwa wakulima, CCM itahimiza na kuweka msukumo mkubwa katika suala la upatikanaji wa mbolea iliyo bora na soko la uhakika lenye kuwafaidisha wakulima kutokana na kuuza mazao yao," alisema.

"CCM itaendelea kutumiza wajibu wake kuendelea kuisimamia serikali kuhakikisha inafanya kazi vizuri na kufikia matarajio ya wananchi," alisema Balozi Nchimbi.

Aidha, Balozi Nchimbi alisisitiza kuhusu upendo baina ya wananchi kwa wananchi, wananchi na viongozi na viongozi kwa viongozi kwa kuzingatia kuwa umoja na mshikamano wetu ndio usalama wa Taifa la Tanzania.

"Pendaneni bila kujali itiadi ya vyama vyenu vya siasa, kabila wala dini," alisisitiza Balozi Dk. Nchimbi.

***Imeandikwa na Maulid Mmbaga (Mara) na Halfani Chusi (Rukwa).***

MAKONDA ASHTUKA...

# Aliyelipa kodi milioni 24/- apewa risiti ya milioni 3/-

**Na Beatrice Shayo,** ARUSHA

MWENYEKITI wa Chama cha Wakala wa Utalii Tanzania (TATO), Wilbard Chambulo, amemweleza Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda, alivyolipa kodi ya Sh. milioni 24 kwa Halmashauri ya Jiji, lakini akapatiwa stakabadhi ikionesha amelipa Sh. milioni tatu.

Makonda alikutana na wadau wa utalii mwishoni mwa wiki kwa ajili ya kujadiliana nao mambo mbalimbali zikiwamo changamoto wanazokutana nazo katika utekelezaji majukumu yao.

"Nimewalipa hawa halmashauri Sh. milioni 24, wameniandikia nimelipa Sh. milioni tatu mpaka ninaogopa kwamba hiyo fedha haijaingia serikalini, unajua ni bora tukose wote lakini tulipe kodi," alisema.



Makonda alihoji, "Umelipa Sh. milioni 24, ina maana malipo ya Sh. milioni 21 hayajaingia jiji?

Chambulo alijibu; "Ndio, nina barua hapa inaonesha nimelipa Sh. milioni tatu, ninataka wanirudishie fedha zangu Sh. milioni 21, haiwezekani ninapigika usiku na mchana kusaidia nchi yangu kwa kulipa kodi, hata hizo kodi hawana information (taarifa) nazo kuwa nimelipa."

Makonda akahoji tena: "Ina maana kama umelipa hiyo kodi kwa 'control number' (namba ya malipo) maana yake upo katika sehemu salama, iweje uandikiwe umelipa Sh. milioni tatu?"

Chambulo alisema wanachoomba kwa Makonda ni kusaidiwa kufikisha ujumbe kwa Rais kuwa malipo kwa njia ya mtandao yatapunguza malalamiko.

Makonda alijibu kuwa suala la malipo kwa njia ya mtandao halipaswi kutatuliwa na Rais au Makamu wa Rais, ni jambo la viongozi wa chini kwa sababu mifumo ilishatengenezwa na serikali ili kuwezesha halmashauri kukusanya mapato.

Chambulo alisema changamoto ya mifumo inayotumika na Mamlaka ya Mapato (TRA) kwenye kudai kodi ni miongoni mwa mambo yanayosababisha uombaji na utoaji rushwa kwa kuwa wanatumia nguvu kubwa kudai kodi na tozo.

Alisema changamoto hiyo inawakuta raia wa India ambao wamekuwa wanasumbuliwa kwenye kudaiwa kodi na wakati mwingine wanafungiwa kwenye chumba na kuteswa ili kuweka mazingira ya kutoa rushwa.

Makonda alisema maelekezo ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, yako wazi katika ukusanyaji mapato.

"Wenzetu wameyarahisisha maisha na sisi tunataka twende huko ili tupunguze urasimu ambao unatuletea ugomvi, chuki na rushwa," alisema.

Makonda pia alionya maofisa wanaokusanya kodi kwa kufuata wafanyabiashara nyumbani kwao wakiwa katika kundi la watu saba kupeleka barua moja ya kumkumbushia kulipa kodi,. jambo ambalo alisisitiza halikubaliki.

Makonda alitoa ufafanuzi huo baada ya mmoja wa wadau wa utalii kulalamikia kufuatwa nyumbani kwake na gari lenye watu saba kupatiwa barua ya kumkumbusha kufanya malipo.

"Kuna kitu kimenishangaza, yaani gari moja mnajazana watu saba kwenda nyumbani kwa huyo mama kumdai kodi. Kwanini muwe watu saba? Hili sikubaliani nalo, huko ni kutengeneza mazingira ya rushwa," alionya.

Makonda alisema kuna haja kuwapo mazingira rafiki ya ukusanyaji kodi badala ya kusababisha usumbufu kwa wafanyabiashara.

"Kwanini msiweke mfumo rahisi hawa wafanyabiashara wote wanajulikana? Kwanini muda unapofika wa kulipa kodi usimtumie email ya kumkumbushia kulipa kodi badala ya kutumia gari na kurundikana humo kumfuata nyumbani kwake? Mnaongeza gharama, gari liwekwe mafuta na ninyi mpo saba kupeleka barua moja, hiyo barua ina nini mpaka ipelekwe na watu saba?" alihoji.

Mkuu wa Mkoa huyo aliagiza kuundwa kamati maalum ya kufuatilia na kutafuta mwarobaini wa changamoto zinazokabili sekta hiyo muhimu kwa uchumi wa Mkoa wa Arusha.

Moja ya maelekezo aliyotoa Rais Samia Suluhu Hassan kwa Makonda baada ya kumwapisha hivi karibuni, ni kukuza na kuimarisha utalii mkoani Arusha.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### ANTONY KUPIGWA BEI

KLABU ya Manchester United inapanga kumuuza winga wa Brazil, Antony mwenye umri wa miaka 24, msimu wa majira ya joto kwa kiwango "kinachokubalika", huku winga wa Crystal Palace, Michael Olise (22), akiwindwa na United. ***(Rudy Galetti via X)***

### WAN-BISSAKA AIVUTIA INTER

KLABU ya Inter Milan inavutiwa na mlinzi wa Manchester United na England, Aaron Wan-Bissaka mwenye umri wa miaka 26, ikiwa beki wa kulia wa Uholanzi, Denzel Dumfries (27), ataondoka Serie A msimu huu. ***(Gazzetta dello Sport)***

### ARSENAL YATAKA STRAIKA

ARSENAL ina nia ya kuleta mshambuliaji ili kutoa ushindani kwa fowadi wa Brazil, Gabriel Jesus mwenye umri wa miaka 27, na kiungo wa kati wa Ujerumani, Kai Havertz (24), huku fowadi wa Bologna, Mholanzi Joshua Zirkzee mwenye miaka 22, akiwa miongoni mwa walengwa wao wakuu. ***(TeamTalk)***

### AMORIM NA LIVERPOOL

KOCHA wa Sporting Lisbon, Ruben Amorim, atapewa muda wa kutekeleza mtindo wake wa uchezaji Liverpool iwapo atakuwa kocha wao mpya. ***(Football Insider)***

### UNITED YAMTAKA TONEY

KLABU ya Manchester United imeibuka kuwa moja ya timu inayoweza kumsajili mshambuliaji wa Brentford na England, Ivan Toney, 28. ***(Mirror)***

### EDERSON AWINDWA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur imeripotiwa kuwa tayari kuongeza juhudi zake za kumsajili kiungo wa kati wa Atalanta, Ederson, 22. ***(TeamTalk)***

### HALL KUONDOKA

MLINZI wa England, Lewis Hall mwenye umri wa miaka 19, ambaye yuko kwa mkopo Newcastle United kutoka Chelsea, anatarajiwa kuondoka 'The Blues' msimu huu wa majira ya joto kwa uhamisho wa kudumu kwenda St James' Park. ***(Mirror)***

### GALLAGHER KUSEPA CHELSEA

KIUNGO wa kati wa England, Conor Gallagher, 24, amekubali kwamba atalazimika kuondoka Chelsea msimu huu wa majira ya joto ikiwa hatapewa mkataba mpya kabla ya mwisho wa msimu huu. ***(HITC)***

### PEDRI KUONGEZEWA

BARCELONA inajiandaa kumpa mkataba mpya kiungo wa kati wa Hispania, Pedri, 21, ambaye amekataa ofa ya Paris St-Germain. ***(Fabrizio Romano)***

### GYOKERES ALENGWA ARSENAL

MSHAMBULIAJI wa Sporting Lisbon na Sweden, Viktor Gyokeres, analengwa zaidi na Arsenal, lakini mkataba wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, una kipengele cha kuruhusiwa kuondoka kwa euro milioni 100. ***(Football Transfers)***

## DONDOO SOKA MAGAZETI ULAYA




# MADRID YAKARIBIA UBINGWA LALIGA

**MADRID,** Hispania

AURELIEN Tchouameni alifunga bao la mapema katika kipindi cha pili na kuipa Real Madrid ushindi wa bao 1-0 ugenini dhidi ya Mallorca na kuwafanya wausogelee ubingwa wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga.

**Kwenye mchezo huo wa Jumamosi, Real Madrid iliwapumzisha wachezaji muhimu kabla ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Manchester City keshokutwa, Jumatano.**

Ushindi huo umeifanya Madrid kufikisha pointi 78, pointi nane mbele ya wapinzani wao Barcelona, ambao watawakaribisha katika mechi ya El Clasico kwenye Uwanja wa Bernabeu wikendi ijayo.

"Tunafahamu tulipo wakati huu wa LaLiga, kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, kila mchezo ni kama fainali," alisema kocha wa Madrid, Carlo Ancelotti katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mechi.

### ●●● Ushindi wa Jumamosi umeifanya kufikisha pointi 78, nane mbele ya wapinzani wao...

"Kuwa na faida hiyo ni muhimu sana kabla ya mechi ya Jumapili [Clasico] na hilo kama lengo letu. Nina furaha sana, kushinda hapa daima ni vigumu. Kipindi cha pili tulicheza kwa kiwango cha juu sana."

Tchouameni alifunga bao hilo dakika ya 48 kwa shuti kali kutoka nje ya eneo la hatari ambalo lilichukua nafasi ya beki na kumwacha kipa akiwa hana cha kufanya.

Washindi wa pili wa Copa del Rey, Mallorca wako nafasi ya 15 kwenye msimamo wa LaLiga wakiwa na pointi 31, sita mbele ya eneo la kushushwa daraja.

Ancelotti alitumia mechi ya Jumamosi huko Mallorca si tu kuwapumzisha wachezaji muhimu kama vile Vinicius Junior, Rodrygo na Toni Kroos, lakini pia aliwaanzisha Nacho na Antonio Rudiger. Tchouameni anatumikia adhabu hatacheza dhidi ya Man City.

Nacho na Rudiger walionekana imara dhidi ya Mallorca katika mechi ambayo Madrid walipaswa kushinda kwa tofauti kubwa zaidi ya mabao.

"Sijawapumzisha wachezaji kwa sababu za kimwili, timu yote iko sawa, ni Rodrygo pekee hakuwa sawa kwa asilimia 100, lakini wengine walikuwa sawa," aliongeza Ancelotti.

"Brahim Diaz alicheza mchezo wa kuvutia, Lucas Vazquez, Luka Modric walifanya vizuri sana. Kimwili timu iko sawa. Tutashinda Jumatano kwa mtazamo wetu, si kwa sababu ya hali yetu ya kimwili."

Jude Bellingham alipata nafasi nzuri zaidi katika kipindi cha kwanza wakati shuti lake lilipotoka nje ya goli. Baada ya Tchouameni kufunga, Madrid walipoteza nafasi kadhaa za kuendeleza uongozi wao, ambao ulijumuisha Diaz kukosa nafasi.

## HABARI MICHEZO




# GUARDIOLA: TUNAWANIA MATAJI MA3

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola aliipongeza timu yake kwa kuwa 'hai' kwenye mbio za kuwania mataji matatu kwa mara nyingine - na ametoa wito kwa wachezaji wake kuchangamkia fursa ya 'ajabu' ya kupambana kwa nguvu zote.

City iliichapa Luton mabao 5-1 na kukaa kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu England Jumamosi (kabla ya mechi za jana Jumapili) kwa mara ya kwanza tangu Novemba, huku tahadhari sasa ikielekezwa kwa Real Madrid kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya Jumatano kabla ya nusu fainali ya Kombe la FA dhidi ya Chelsea.

Alipoulizwa kuhusu jinsi timu yake inavyopanda msimu unapofika hatua za mwisho, alisema, inashangaza kuwa hapa tena.

"Baada ya kumaliza msimu uliopita bado tunapambana kwenye Ligi Kuu tukiwa tumebakisha pointi 21.

"Jumatano tunacheza na Real Madrid tukiwa na nafasi ya kufuzu kwa nusu fainali na nguvu zote zitaletwa na mashabiki wetu.

"Na Kombe la FA Jumamosi ijayo dhidi ya Chelsea, tena nusu fainali. Ni pendeleo lililoje.

"Kwa hiyo jaribu kuongeza kwa wiki moja zaidi na wiki moja zaidi. Kwenye Ligi Kuu tuna wiki moja zaidi. Tunayo nafasi.

"Sijui nini kitatokea kesho, lakini hakuna ushindi leo, wanashinda. Lazima tushinde michezo yetu na kuwafanya Arsenal na Liverpool kuhisi shinikizo. Huu ndio ujumbe pekee tunaoweza kufanya na mechi sita zimebakia. Tumefanya kazi yetu."

# Ten Hag bado ana matumaini kufuzu Uefa




**BOURNEMOUTH,** England

KOCHA Erik ten Hag, amekataa kwamba Manchester United ipo nje ya mbio za kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao baada ya timu hiyo kutoka sare ya mabao 2-2 na Bournemouth Jumamosi.

United, ambao wameshinda mechi moja tu kati ya saba zilizopita katika michuano yote, wako pointi 10 nyuma ya Aston Villa walio nafasi ya nne na Tottenham Hotspur walio nafasi ya tano huku kukiwa na michezo sita iliyobakia katika kinyang'anyiro cha kuwania kufuzu kwa Ligi ya Mabingwa msimu ujao.

"Tunatoa tunachoweza, lakini pia nina ukweli," alisema Ten Hag akiwaambia waandishi wa habari baada ya filimbi ya mwisho ya mchezo huo.

"Na kwa hivyo wakati kikosi kamili kilikuwapo, bado ningesema imani kubwa, lakini tutaendelea kupambana na wachezaji wanaopatikana. Na unaona kuna uwezo wa juu lakini pia wachezaji wachanga.

"Ndio, wanafanya makosa na kama watalazimika kufanya kila mechi ya Ligi Kuu na wamethibitisha kuwa wanaweza kushindana na timu bora katika kiwango cha juu. Walithibitisha. Lakini sasa wanapaswa kufanya hivyo mara kwa mara na hilo ndilo linalofuata kila mara, hatua kwa wachezaji wachanga."

Alipoulizwa kama anakubali kwamba Ligi ya Mabingwa iko nje ya timu yake sasa, Ten Hag alisema: "Hapana. Hapana, sikusema hivyo."

Kushindwa kwa United kuifunga Bournemouth, na ushindi wa 4-0 wa Newcastle United dhidi ya Tottenham mapema Jumamosi, ulimaanisha kwamba timu ya Ten Hag ilishuka hadi nafasi ya saba kwenye msimamo.

Ten Hag alikataa kujibu swali alipoondoka kwenye mkutano na wanahabari kuhusu uwezekano wa United kushuka hata chini kwenye msimamo.

Iwapo United itamaliza msimu katika nafasi ya nane au chini, utakuwa mwisho mbaya zaidi kwao katika historia ya Ligi Kuu ya England.

"Sichukui suala hilo," alisema Ten Hag. "Hilo si muhimu kwa wakati huu."

# Utakatifu sana umeua ndoa na Kaka - Mke

**RIO DE JANEIRO,** Brazil

MKE wa zamani wa mchezaji wa Kimataifa wa Brazil, Kaka, amefichua sababu ya ajabu iliyomfanya kuomba talaka mwaka 2015 baada ya miaka 10 ya ndoa yao, kwamba mume wake alikuwa mtakatifu sana.

Kaka mwenye umri wa miaka 41, alifurahia maisha mazuri katika Klabu za Sao Paulo, AC Milan, Real Madrid na Orlando City, kabla ya kustaafu mwaka 2017. Mnamo mwaka 2005, wakati alipokuwa aking'ara AC Milan, Kaka alifunga ndoa na mpenzi wake wa utotoni, Caroline Celico.

Katika ndoa yao wana Watoto wawili, wa kiume na wa kike, lakini walitangaza kwenye mitandao ya kijamii kuwa walitengana mnamo 2015 baada ya miaka 10 ya ndoa. Na, kama ilivyoripotiwa na gazeti la The Sun, Celico ambaye ameolewa tena - alielezea kwa nini aliamua kutengana na mumewe.

"Kaka hakuwahi kunisaliti," alisema.

"Alinitendea vizuri, alinipa familia nzuri, lakini sikuwa na furaha, kuna kitu kilikosekana.

"Tatizo lilililokuwapo ni kwamba, Kaka alikuwa mkamilifu sana kwangu (mtakatifu mno)."

Kaka anajulikana kama Mkristo mwaminifu mno na wakati wa ndoa yao Celico alijiunga na kanisa la nyota huyo wa soka, kabla ya kuwa mchungaji wa Kiinjili.

Aliacha jukumu hilo mwaka wa 2010 na kuanzisha Horizontal Love, shirika la hisani ambalo hutoa vifaa vya chakula, usafi, ujenzi na elimu kwa mashirika yasiyo ya kiserikali ya Brazil.

Baada ya kutengana kwao, Kaka sasa anaishi na mpenzi wake mpya Carolina Dias tangu mwaka 2017. Wawili hao walitangaza uchumba mapema mwaka huu, huku Kaka pia akiwa na mtoto wa kike mwenye umri wa mwaka mmoja na mwanamitindo huyo wa Brazil.

Maisha ya Kaka yaliyopambwa sana kwenye mchezo huo yalimfanya kushinda mataji 12, likiwamo Ligi ya Mabingwa Ulaya na Kombe la Dunia, huku pia akifunga mara 29 katika mechi 92 alizoichezea Brazil.



HABARI MICHEZO

# Kampuni yasaka vipaji vya muziki shuleni

Na Mwandishi Wetu

KAMPUNI ya School Star Search Africa Limited imezindua programu yake mpya ya kusaka vipaji shuleni.

Uzinduzi huo ulifanyia juzi katika Kijiji cha Makumbusho, Dar es Salaam, ukiambatana na kushindanisha vijana 12 kutoka shule za sekondari za mkoa huo. Programu hiyo imeanza na shule saba zikiwamo Benjamin Mkapa, Kibasila na Azania.

Mwanzilishi Mwenza wa Kampuni hiyo, Ally Ramadhani alisema kampuni hiyo inahusisha vijana na inalenga kuibua, kuendeleza na kusimamia vipaji vya muziki hasa kwa vijana wadogo ambao ni wanafunzi nchini.

"Kampuni yetu ilianzishwa mwaka 2023, lakini leo (juzi), tupo katika hafla hii ya uzinduzi wa programu yetu ya School Star Search kwa awamu ya kwanza mwaka 2024, lengo hasa ni kuibua vipaji kwa vijana walioko shuleni na kuviendeleza ili wajikomboe katika sekta ya kiuchumi na ajira kwa ujumla.

"Baada ya kupata washindi watano katika hafla hii ya leo (juzi), washindi hao wajumuika nasi katika mashindano ya kitaifa ambayo yanatarajiwa kufanyika Oktoba hadi Desemba mwaka huu, tutakuwa na kinyang'anyiro cha kumpata mshindi wa jumla. Mashindano haya tunategemea yatakuwa na washiriki zaidi ya 100 kutoka shule mbalimbali nchini," alisema.

Mshindi wa kwanza katika uzinduzi huo, Glorious Sabigael ambaye ni mhitimu wa kidato cha nne kutoka Shule ya Sekondari Dar es Salaam mwaka 2023, alihimiza waendeshaji programu hiyo kuendelea kusaka vipaji hivyo kwa vijana walioko shuleni kwa kuwa mashindano mengi yaliyopo kwa sasa nchini huzingatia zaidi vijana walioko vyuoni na wenye umri kuanzia miaka 18.

"Sikutegemea kama leo nitakuwa mshindi lakini ninashukuru Mwenyezi Mungu, nina imani mashindano haya yatazidi kutujengea imani na kujiamini katika kile tulichonacho na kuzidi kutupa nguvu zaidi ya kufikia malengo yetu. Wito wangu kwa wanafunzi wengine wasifiche vipaji vyao kwani ni mtaji na baraka kwetu," alisema Glorious.

Uzinduzi huo ulihudhuriwa na mtayarishaji wa muziki nchini, Paul Maker, ambaye alikuwa jaji mkuu katika mashindano hayo.

# MTANZANIA ASHINDA TUZO YA GLOBAL CITIZEN 2024

Na Mwandishi Wetu

MTANZANIA Lydia Charles Moyo, amekuwa mmoja kati ya washindi sita waliotambuliwa kwa Tuzo ya Shirika la Kimataifa la Global Citizen mwaka 2024, ikionyesha juhudi za vijana ulimwenguni katika kuleta mabadiliko.

**Kwa mujibu wa taarifa, uthabiti wake usio na kifani katika kukabiliana na umasikini na kuwezesha kiuchumi kwa wasichana na wanawake vijana ndiyo umeleta utambuzi huu wenye heshima duniani, na kumweka pamoja na kikundi cha vijana wachache kinachong'ara miongoni mwa mamilioni ulimwenguni kote.**

Hata hivyo, kwa mujibu wa tovuti ya Shirika la Her Initiative, ambalo Lydia ni Mkurugenzi na mwanzilishi wake, lilianzishwa miaka mitano iliyopita ambapo kupitia shirika hilo linaloongozwa na wanawake vijana, Lydia hutekeleza miradi inayolenga kuwawezesha kifedha wasichana na wanawake vijana, kuchagiza matumaini na fursa mahali ambapo wasichana na wanawake wamekata tamaa.

Akizungumzia utambuzi huo, Lydia ameishukuru timu ya Her Initiative, washirika, wafadhili, na wafuasi wa kazi zake, wote wa ndani ya Tanzania na kimataifa. "Tuzo hii inamaanisha mengi kwangu na kazi tunayofanya na Shirika la Her Initiative. Inathibitisha uimara na azimio la wanawake na wasichana vijana, ambao wana ndoto na malengo makubwa na wanafanya kazi kwa bidii ili kuboresha si tu maisha yao binafsi, bali pia ya jamii zao," alisema na kuongeza.

Akizungumzia ombwe kubwa la kijinsia katika upatikanaji wa uchumi, Lydia alisisitiza umuhimu wa kazi wanayofanya na Her Initiative. Kwa kutumia mikakati na mbinu mbalimbali za uwezeshaji kiuchumi na kwamba Her Initiative wanakusudia kuvunja mzunguko endelevu wa umaskini na kuimarisha uwezo wa kiuchumi kwa wasichana na wanawake vijana wa Kitanzania.

Alisema kiini cha mikakati yao ni uwezeshaji kiuchumi na uvumbuzi wa kiteknolojia, kama ilivyoonyeshwa na jukwaa la kielimu la 'Panda Digital' ambalo ni la kujifunza mtandaoni linalotumia kiswahili na tayari limewawezesha zaidi ya wasichana na wanawake 5,000 kote Tanzania kupata ujuzi muhimu wa masoko na biashara, huku pia likiwawezesha kuunganishwa na fursa na mtandao muhimu kuanzisha na kukuza biashara zao.

Kupitia taarifa kwa vyombo vya habari iliyochapishwa na Global Citizen, Liza Henshaw, Rais wa Global Citizen, amesisitiza jukumu muhimu la uongozi wa vijana katika kuleta mabadiliko halisi.

Anna Kulaya ambaye ni miongoni mwa wajumbe wa Bodi ya Ushauri ya Shirika la Her Initiative, alisema hamasa ya Lydia haina ufananisho na dunia inapaswa kuwaunga mkono viongozi wanawake wenye uthubutu kama yeye.

Washindi wa Tuzo ya Global Citizen mwaka 2024 watatambuliwa wakati wa mkutano wa 'Global Citizen NOW' hapo Mei Mosi na 2, mwaka huu huko New York, Marekani.

Global Citizen ni Shirika la Utetezi na Uchechemuzi la Kimataifa linalopigania kumaliza umaskini. Kwa msaada wa jamii ya kimataifa ya watetezi wa kila siku wanaopaza sauti zao na kuchukua hatua, juhudi zao zinapata nguvu kupitia kampeni na matukio yanayokusanya viongozi katika muziki, burudani, sera za umma, vyombo vya habari, hisani, na sekta ya biashara.

Katika kipindi cha muongo mmoja, Global Citizen imefanikisha ahadi za zaidi ya dola bilioni 43.6, ikichochea miradi ya mageuzi ambayo imegusa maisha ya watu takriban bilioni 1.3 ulimwenguni. Mafanikio haya yanathibitisha nia ya shirika hilo kutimiza ulimwengu usio na umaskini, huku likiashiria nguvu ya hatua ya pamoja katika kuendesha maendeleo kwa kiwango cha kimataifa.




Mshindi wa Tuzo ya Shirika la Kimataifa la Global Citizen kwa mwaka 2024, Lydia Moyo, akizungumza na vyombo vya habari jijini Dar es Salaam wiki iliyopita. **MPIGAPICHA WETU**

# *Vifaa vitano vipya Simba hivi hapa*

INATOKA UKURASA 24

Inonga yupo sokoni muda wowote anaweza kupigwa bei," kilidokeza chanzo hicho.

Aliongeza kuwa kabla ya msimu huo kumalizika Benchikha atakutana na Mwekezaji Mohamed 'Mo' Dewji kwa ajili ya kufanya tathimini ikiwamo wachezaji watakaochwa na wakuongezwa msimu ujao.

Kwa mujibu wa mwekezaji huyo, atakutana na Benchikha kujadili na kufanya tathimini ya timu yao na kuangalia nani wa kumtema na wakumuongeza kulingana na mapendekezo yake.

Katika hatua nyingine Kocha Msaidizi wa Simba, Selemani Matola, amesema wana kazi kubwa hususan katika safu ya ushambuliaji ambayo imekuwa ikishindwa kuzitumia nafasi wanazotengeneza.

Alisema wameumizwa kupoteza pointi mbili mbele ya Ihefu FC, kwa sababu wamecheza mpira mzuri na kumiliki huku wakitengeneza nafasi, lakini wameshindwa kuzitumia na kupoteza alama mbili.

"Tatizo letu liko pale pale, kushindwa kutumia nafasi, ukiangalia Freddy (Michael) angekuwa makini tungepata matokeo, tunaenda kujiuliza na kufanyia kazi makosa hayo tukijiandaa na mchezo wetu dhidi ya Yanga.

Bado tupo katika mbio za ubingwa hatujakata tamaa na tunaenda kujipanga kwa ajili ya kusaka pointi tatu katika mchezo wetu wa Derby, ninaimani tutafanya vizuri," alisema Matola.

Mechi ya watani wa jadi inatarajia kuchezwa Jumamosi wiki hii katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam huku Yanga ikiwa wenyeji wa mchezo huo.

Michezo

Jumatatu Aprili 15, 2024

Nipashe



Ten Hag bado ana matumaini Uefa UKURASA 22

# YANGA SC, AZIZ KI WANOGA KILELENI

Na Adam Fungamwango

MABAO mawili ya Muivory Coast, Joseph Guede na moja la Mburkina Faso, Stephane Aziz Ki, jana yaliwapa Mabingwa Watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Singida Fountain Gate na kuiongezea mbio za ubingwa.

**Lakini pia ushindi huo ni ishara ya salamu kwa watani zao wa jadi, Simba watakaokwenda kukutana nao Jumamosi ijayo, Uwanja wa Benjemin Mkapa, Dar es Salaam.**

Katika mechi hiyo iliyochezwa Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza, ilishuhudia Clement Mzize akitoa pasi mbili za mabao 'asisti', huku Aziz Ki akiongeza bao moja na kufikisha 14, akikaa kileleni mwa orodha ya wafungaji wa Ligi Kuu na kumuacha Feisal Salum, 'Fei Toto' mwenye mabao 13.

Haikuwa mechi yenye ufundi sana kutokana na uwanja kuwa na matope na maji yaliotuama kwenye maeneo mengi uwanjani, kiasi cha kusababisha wachezaji kucheza kwa wanavyojua wao, lakini si kwa kutumia mifumo ya makocha wao.

Wachezaji wa timu zote mbili walionekana wakiteleza na kuanguka wanapokimbilia mpira, au wanapopigwa chenga.

Dakika ya kwanza tu, Yanga ilianza kulitia msukosuko lango la Singida Fountain Gate dakika ya kwanza tu, wakati Clement Mzize alipotanguliziwa mpira kwa Jonas Mkude, lakini akiwa ana kwa ana na kipa Benedict Haule, shuti lake lilitoka nje.

Nicolaus Gyan, mchezaji wa zamani wa Simba, alijibu shambulizi hilo dakika ya pili kwa shuti kali nje ya eneo la hatari, lakini mpira ukapaa juu ya lango.

Haule, alifanya kazi ya ziada kwa timu yake, alipotema shuti kali la Maxi Nzengeli alilolipiga akiwa ndani ya boksi, na mpira huo kwa sababu ulikuwa na nguvu bado ulikuwa unaelekea wavuni, lakini aliurukia na kuudaka ukiwa haujavuka mstari wa lango.

Kwa mara nyingine tena, Mzize aliikosesha Yanga bao dakika ya 33, alipounganisha kichwa ambacho hakikulenga lango, alipoletewa pasi ya juu na Nzengeli. Yanga ilifanikiwa kuandika bao dakika ya 41, lililofungwa na straika Guede, raia wa Ivory Coast, aliyesajiliwa kipindi cha dirisha dogo.

Aliupata mpira mrefu uliopigwa kutoka katikati ya uwanja, na akiwa pembeni kwenye wingi ya kushoto, alimpindua nahodha wa Singida Fountain Gate, Biemez Carno, raia wa Jamhuri ya Kidemkorasi ya Congo, akapiga shuti lililombabatiza kichwani beki, Idd Habib, mpira ukampoteza maboya kipa Haule, na kujaa wavuni.

Bao la pili la Yanga liliwekwa wavuni na Aziz Ki dakika ya 65 kwa shuti kali la mbali kiasi cha mita 30 kwa mguu wa kushoto ambalo lilimkuta kipa Haule akiwa hajajiandaa na kujaa wavuni.

Dakika tatu baadaye, Guede alipachika bao la tatu kwa Yanga na la pili kwake kwa kichwa maridadi, baada ya kazi nzuri iliyofanywa na Mzize.

Kazi kubwa ilianza kufanywa na mfungaji mwenyewe alipata mpira toka nyuma kwa Khalid Aucho, akakimbia nao umbali mrefu, kabla ya kumpa Mzize ambaye alimuacha mfungaji kukaa kwenye eneo zuri na kumrudishia mpira.

Yanga imefikisha pointi 55 kwa michezo 21 iliyocheza, ikiendelea kupunga hewa kileleni mwa msimamo, huku Singida Fountain Gate ikishuka kutoka nafasi ya nane hadi ya tisa, ikibaki na pointi zake 24, ikiwa imecheza mechi 22.

## Watuma salamu Simba, huku Fei Toto akitimuliwa vumbi mbio za ufungaji...



Stephane Aziz Ki (mgongoni), akimpongeza Joseph Guede na kushangilia naye baada ya kuifungia Yanga bao la kwanza dhidi ya Singida FG, kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa CCM Kirumba jana. Yanga ilishinda mabao 3-0. **MPIGAPICHA WETU**

## Vifaa vitano vipya Simba hivi hapa

Na Saada Akida

WAKATI Simba ikijiandaa kwa Derby ya Kariakoo, dhidi ya Yanga Aprili 20, mwaka huu, uongozi wa klabu hiyo umeanza kuingia chimbo na kusaka nyota wa kuwasajili huku majina ya baadhi ya majina ya wachezaji watano ambao tayari mazungumzo yameanza, yakifahamika.

Simba imekuwa katika presha kubwa kutokana na timu yao kutofanya vizuri baada ya kutupwa nje kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika na kisha kutolewa katika michuano ya CRDB Federation Cup, maarufu Kombe la FA, huku ikianza kuwa na mwendelezo mbaya Ligi Kuu Bara.

Nyota wanaotajwa mambo kuwa mazuri katika mazungumzo yao na Simba ni Chickna Diekite anacheza winga wa kushoto katika Klabu ya Real Bamako ya nchini Mali, Derrick Fordjour kutoka Klabu ya Medeama SC ya Ghana, mshambuliaji Foday Trawelly kutoka Brikama United na Rodger Torach kutoka klabu ya Vipers ya Uganda anacheza beki.

Kadhalika Simba inadaiwa imepeleka ofa kwa uongozi wa Singida Fountain Gate FC kuhitaji saini ya Nickson Kibabage ambaye anacheza Yanga kwa mkopo ambao unaisha mwishoni mwa msimu huu.

Taarifa kutoka ndani ya Bodi ya Wakurugenzi ya Simba, tayari majina hayo yapo mezani kwa ajili ya kujadiliwa kutokana na nafasi ambazo zimependekezwa na Kocha Abdelhak Benchikha kuboreshwa.

Imeelezwa kuna baadhi ya wachezaji ambao kocha anawahitaji kwa kutaja nafasi hivyo, kazi kubwa imefanywa na skauti kuangalia aina ya wachezaji na kwamba wapo wengi wanaotarajiwa kutemwa mikataba yao ikimalizika.

"Kuna wachezaji ambao msimu ujao hawatakuwa sehemu ya kikosi akiwamo Saido Ntibazonkiza mkataba wake unafika ukingoni, Aubin Kramo huenda akaenda kwa mkopo Zesco ya Zambia na Henock

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >